# OFISI YA MAKAMU WA RAIS
## WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

NA. 00000394

TOLEO LA 45 - DESEMBA 2023




# MAKAMU WA RAIS achagiza upandaji miti kuadhimisha Mapinduzi ya Zanzibar


*Jarida hili limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania*

Ofisi ya Makamu wa Rais blog.vpo.go.tz

www.vpo.go.tz




**Bodi ya Uhariri**

Sigsbert Kavishe
Paul Masanja
Paulo Laiser
Mugisha Kyamani
Ismail Ngayonga
Joyce Mnunguli
Daniel Sagata
Zanipha Msangi

**Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Ofisi ya Makamu wa Rais**
S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 266 235 2038
Nukushi +266 235 0002
Barua pepe: km@vpo.go.tz
Tovuti: www.vpo.go.tz
Ofisi ya Makamu wa Rais
blog.vpo.go.tz

# Tahariri

Jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais toleo namba 45 limeandaliwa kwa ajili ya kuhabarisha na kuelimisha wasomaji na umma kwa ujumla kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na Hifadhi ya Mazingira.

Toleo hili linatoa dondoo kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ambazo zimeainishwa katika habari na picha za matukio yaliyotokea katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2023.

Aidha, toleo hili linatoa muhtasari kuhusu ziara mbalimbali zilizofanywa na Viongozi Waandamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais ndani na nje ya nchi ikiwa ni juhudi za Serikali za kuhamasisha jamii kushiriki katika kudumisha Muungano na kuhifadhi mazingira.

Kupitia toleo hili, ndugu msomaji utahabarika na kuelimika kwa kina kupitia habari, Makala na picha zinazoakisi majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Habari, makala na picha hizo zinahusisha ziara mbalimbali za Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akitekeleza majukumu mbalimbali kwa kutoa maelekezo na maagizo kwa viongozi na watendaji wa Serikali.

Aidha jarida hili linaakisi kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) waliokutana kujadili masuala ya Muungano, Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023.

Halikadhalika jarida liaeleza ushirikiano na juhudi zilizopo baina ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serkali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) katika kutekeleza miradi ya hifadhi ya mazingira ambayo imesaidia kuboresha kipato na ustawi wa wananchi wa pande zote mbili.

Ni matumaini yetu msomaji utapata habari na elimu kuhusu shughuli zilizofanyika katika Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ina dhamana ya kusimamia hifadhi ya mazingira na kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

***#Kazi Iendelee!***



Dkt. Mpango ataka ufanisi wa katazo la matumizi plastiki Uk. 4



Dkt. Jafo awaasa Watanzania kuuenzi Muungano kwa kudumisha amani Uk.31



Tanzania, Japan zateta ufadhili miradi ya mazingira Uk. 28



Zanzibar kunufaika na Biashara ya Kaboni Uk. 29



Katibu Mkuu Maganga awataka watafiti kuweka mipango ya matumizi ya rasilimali za bahari Uk. 44



Mitawi: Maafisa Ununuzi zingatieni miongozo ya ununuzi wa vifaa Uk. 70



Pinda atoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kutangaza fursa za Biashara ya Kaboni Uk. 74

Kitabu cha Muungano kuanza kutumika mashuleni Uk. 36

Makamu wa Rais aifungulia milango Qatar kuwekeza katika teknolojia kukabili mabadiliko ya tabianchi Uk. 17

Dkt. Jafo: Fanyeni tafiti zitakazotoa ufumbuzi wa mabadiliko ya tabianchi Uk. 45

Tanzania yasisitiza Mikakati Hifadhi ya Bionuai Mkutano wa GEF Uk. 55



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akihutubia Viongozi na Wananchi mbalimbali wa Mkoa wa Dodoma mara baada ya kuongoza zoezi la kufanya usafi katika Soko Kuu la Wamachinga mjini Dodoma ikiwa ni Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Juni 05, 2023.*

# Dkt. Mpango ataka ufanisi wa katazo la matumizi plastiki

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amelitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuongeza nguvu zaidi katika kusimamia utekelezaji wa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini.

Makamu wa Rais ametoa maagizo hayo mara baada ya kuongoza zoezi la kufanya usafi katika soko kuu la Wamachinga jijini Dodoma ikiwa ni katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani Juni 05, 2023.

Amesema ni lazima kuhakikisha hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wanaokiuka maagizo hayo pamoja na kuwataka watendaji wote wanaohusika kusimamia kwa karibu uzalishaji na matumizi ya mifuko mbadala.

Dkt. Mpango ameongeza ni vema kuhakikisha mifuko yote inayozalishwa inaonesha taarifa za mzalishaji na kama inakidhi viwango vilivyowekwa na mamlaka husika. Pia amesisitiza kampuni na watu binafsi wanaozalisha bidhaa za plastiki kuhakikisha taka zinazotokana na bidhaa zinazozalishwa zinakusanywa na kuondolewa.

Amekemea utoaji wa tenda za uzoaji taka kwa kampuni zisizokuwa na uwezo na zile zisizo na vitendea kazi vya kisasa na kuzitaka Halmashauri kuweka miundombinu ya uhakika ya ukusanyaji na usombaji wa taka katika mitaa na maeneo ya mikusanyiko kama sokoni, stendi na hospitalini.

Aidha Dkt. Mpango ametoa wito kwa wananchi kutambua wajibu walionao katika kutunza vyanzo vya maji, kuacha mazoea ya kutupa taka hovyo na kuagiza kila kaya kuwa na sehemu mahsusi ya kuhifadhia ama kuchomea taka. Amesema suala la kufanya usafi na utunzaji mazingira hayana mbadala kwa kuwa mazingira ndio uhai na yana mahusiano ya moja kwa moja na ustawi wa Taifa kiuchumi na kijamii.

Itakumbukwa kuwa mwaka 2019 wakati Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuwa Makamu wa Rais, Serikali ilianzisha Kampeni kubwa ya kusitisha matumizi ya mifuko ya plastiki nchi nzima na kuagiza itumike mifuko mbadala ambayo ni rafiki zaidi kwa mazingira yetu.

Kampeni hiyo ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa, na Tanzania ilisifika kimataifa kuwa miongoni mwa nchi zilizofanikiwa kupunguza taka za plastiki.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dkt. Selemani Jafo



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akiongoza Viongozi na Wananchi mbalimbali wa Mkoa wa Dodoma kufanya usafi katika Soko Kuu la Wamachinga jijini Dodoma ikiwa ni Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Juni 05, 2023. Kulia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo.*

amesema suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira limeendelea kupewa kipaumbele hapa nchini ambapo kwa kutumia Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Kaulimbiu iliyokuwa na lengo la kuhamasisha ajenda ya utunzaji wa mazingira na kutunza vyanzo vya maji.

Dkt Jafo amewapongeza wanafunzi wa shule za msingi hadi vyuo vikuu kwa kuhifadhi mazingira ikiwemo kampeni ya soma na mti yenye lengo la kuhamasisha upandaji wa miti mashuleni. Halikadhalika amewashukuru wadau mbalimbali katika jitihada zao za kuhakikisha suala la mazingira linapewa kipaumbele kwa maendeleo endelevu.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule amesema Mkoa huo unaendelea na kampeni ya kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki ambapo tayari kwa kushirikiana na NEMC waliweza kukifungia kiwanda kimoja kinachozalisha mifuko hiyo. Amesema elimu inaendelea kutolewa katika masoko na maeneo mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wanaachana na matumizi ya mifuko hiyo.

Pia ameongeza kwamba Mkoa huo utaendelea na jitihada za kulinda vyanzo vya maji ikiwemo chanzo cha maji Mzakwe kwa kusimamia na kupanda miti katika eneo hilo muhimu. Amesema mkoa utaendeleza hamasa ya usafi wa mazingira iliofanyika katika wiki ya kuadhimisha siku ya mazingira duniani hususani usafi katika mifereji ya jiji la Dodoma.

Zoezi la kufanya usafi katika soko kuu la Wamachinga jijini Dodoma limewashirikisha viongozi mbalimbali, wananchi na watumiaji wa Soko hilo. Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kwa mwaka 2023 inasema ***"Pinga uchafuzi wa mazingira utokanao na mifuko ya plastiki"***



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akisukuma toroli alilotumia kukusanya takataka mara baada ya kuongoza zoezi la kufanya usafi katika Soko Kuu la Wamachinga mjini Dodoma ikiwa ni Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Juni 05, 2023.*



# Makamu wa Rais ahutubia Mkutano wa 78 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema kwa sasa dunia inashuhudia kufifia kwa mshikamano thabiti wa kihistoria, udugu na kujitolea, kutoingiliana, usawa baina ya mataifa na kunufaishana uliowekwa na waanzilishi wa Umoja wa Mataifa.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati akihutubia Mkutano wa 78 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa jijini New York nchini Marekani Septemba 22, 2023.

Amesema ili kurejesha imani na mshikamano baina ya mataifa ni vema mataifa yaliyoendelea kuhakikisha yanatimiza ahadi zake na sauti za mataifa yanayoendelea zinasikilizwa.

Amesema kumekuwepo na kutoaminiana baina ya mataifa na hivyo kupelekea mmomonyoko wa utawala wa sheria, mataifa kuunda miunganiko tofauti na ile ya asili pamoja na kurejea kwa maamuzi ya upande mmoja. Ameongeza kwamba kwa sasa kumekuwa na maswali zaidi juu ya ufanisi wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa pamoja na Taasisi za Fedha za kimataifa zikihitajika kufanyiwa maboresho ya haraka.

Makamu wa Rais amesema Umoja wa Mataifa unapaswa kuwakemea kwa uwazi wale wote wanaoshiriki katika kuchochea migogoro barani Afrika kwa lengo la kuuza silaha au kupata utajiri wa rasilimali zilizopo. Ameongeza kwamba dunia inahitaji kuwekeza zaidi katika mazungumzo na diplomasia katika kutatua migogoro ya kivita ili kuifanya kuwa sehemu salama kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Halikadhalika Makamu wa Rais amesema Tanzania itaendelea kuchangia katika juhudi za kuleta na kudumisha amani barani Afrika na kwingineko duniani na kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuongeza uungaji mkono katika mipango ya kikanda ya kuleta amani katika maeneo yenye vita barani Afrika. Amesema hadi kufikia mwezi machi 2023 Tanzania imekua ndio mchangiaji mkubwa wa 12 kati ya nchi 125 katika shughuli za Umoja wa Mataifa za kulinda amani.

Makamu wa Rais amesema utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu umekuwa wa kukatisha tamaa hasa kutokana na kutotekelezwa kwa ahadi za kifedha na teknolojia kutoka kwa nchi zilizoendelea duniani na upungufu wa fedha katika nchi nyingi za Afrika.

Amesema Tanzania imedhamiria kutekeleza kikamilifu malengo ya maendeleo enedelevu kama inavyotarajiwa ambapo Julai mwaka huu iliwasilisha Ripoti ya pili ya Hiari ya Taifa (VNR) ambayo inaonyesha kwa ujumla kumekuwa na mafanikio makubwa kwa lengo namba 2 – 7 kwa ongezeko la uwiano wa kutosha wa chakula, upatikanaji wa dawa muhimu, kupungua vifo vya chini ya miaka 5,hatua muhimu katika kuhamasisha usawa wa kijinsia, uboreshaji wa upatikanaji wa maji mijini na vijijini pamoja na utoaji wa huduma ya nishati ya umeme.

Ameongeza kwamba pamoja na kuwepo kwa utendaji wa wastani katika lengo namba 1,8 na 10, Tanzania imedhamiria kuchukua hatua kuboresha zaidi juhudi za mapato ya ndani huku ikitumia mfumo wa ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi pamoja na kuweka kipaumbele kwenye uwekezaji katika sekta za huduma za jamii, kilimo na biashara ya kilimo, uongezaji thamani na miundombinu, pamoja na kuinua ujuzi wa vijana.

Kuhusu mazingira, Makamu wa Rais amesema Tanzania inasisitiza wito wake wa kuchukua hatua za haraka na za pamoja za kupunguza uzalishaji wa gesijoto pamoja na kuimarisha hatua za kukabiliana na hali hiyo.

Amesema ni lazima kuweka mazingira wezeshi na kuwezesha uwekezaji unaohitajika ili kutumia rasilimali kwa ajili ya kuongeza utekelezaji wa ahadi zinazohusu mabadiliko ya tabianchi na uondoaji wa kaboni katika uchumi wa dunia. Aidha amesema Tanzania inasisitiza wito wake wa mabadiliko ya haki katika kufikia nishati safi kwa nchi za Afrika.

Makamu wa Rais amesema Tanzania imeendelea kuwa imara katika kupinga dhuluma popote inapotendeka na kwa yeyote yule. Ametoa wito wa kuondolewa kwa vikwazo vya kiuchumi visivyo vya haki kwa mataifa kwani vimekua vikidhoofisha uhuru na ustawi kwa wote.

# Dkt. Jafo awahimiza Wakuu wa Mikoa kusimamia usafi wa mazingira



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza wakati wa Mafunzo ya Uongozi kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa (picha ya chini) yaliyofanyika Agosti 26, 2023 mjini Kibaha Mkoani Pwani.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo ametoa rai kwa Wakuu wa Mikoa kuifanya ajenda ya usafi wa mazingira kuwa ya kudumu.

Ametoa wito huo Agosti 26, 2023 wakati akizungumza katika Mafunzo ya Uongozi kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa yaliyofanyika katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere iliyopo Kibaha mkoani Pwani.

Dkt. Jafo amewataka Wakuu hao wa Mikoa kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo chini yao kusimamia vyema zoezi la usafi wa mazingira katika maeneo yao ili kuifanya miji kuwa safi.

Amesisitiza kuwepo na utaratibu maalumu wa kuanzisha utaratibu maalumu wa huduma za kijamii (vyoo vya kisasa na hoteli) kwa abiria wanaosafiri kwa mabasi badala ya porini kama unavyofanyika kwa baadhi ya mabasi hali inayosababisha uchafuzi wa mazingira.

Aidha, Waziri Jafo amewataka Wakuu wa Mikoa hao kusimamia suala la upangaji wa miji katika maeneo yao ili uwekezaji usikwame kutokana na changamoto za kimazingira.

Amesema kuwa bila kupanga miji vizuri uwekezaji unakuwa ni changamoto kubwa kwani itawalazima wawekezaji kusubiri kupata Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) kabla ya kuanza hatua ya ujenzi wa miradi.

"Mtu atataka kujenga kiwanda katika makazi ya watu, mambo yanakuwa yanaingiliana na mwisho wa siku wakati mwingine EIA zinachelewa kwa sababu tumeshindwa kufuata utaratibu wa mipango miji hivyo, tuwasisitize watu wetu wa mipango miji kuhakikisha wanapanga vizuri miji yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi," amesisitiza.

Kwa upande mwingine Waziri Dkt. Jafo amewahimiza viongozi hao kuendelea kusimamia zoezi la upandaji wa miti milioni 1.5 kwa mwaka katika kila halmashauri wanazozisimamia ili hifadhi ya mazingira iwe endelevu.



# Serikali yaweka mikakati kurejesha uoto wa asili

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imesema imeendelea kuweka mikakati na mipango mahsusi ili kuhakikisha inarejesha uoto wa asili katika ardhi takribani hekta milioni 5.2 ifikapo mwaka 2030.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga wakati akifungua warsha ya Programu ya Urejeshaji ya kidunia (TRI), kutoka mataifa 10 duniani inayotekeleza Mradi wa Urejeshaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai Ulimwenguni, iliyofanyika Novemba 6, 2023 jijini Dar es Salaam.

Maganga amesema uchumi wa Tanzania kwa kiasi kikubwa unategemea maliasili ikiwemo misitu, bahari, maziwa, mito, ardhi oevu, wanyamapori na ardhi ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini, hata hivyo matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali hizo yameleta tishio la uwepo wa rasilimali hizo.

"Upotevu wa bioanuai ikiwa ni pamoja na viumbe wengine wa majini unachochewa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu ikiwemo kilimo na matumizi mengine ya ardhi yasiyo endelevu.... Tumeanzisha programu mbalimbali za urejeshaji wa uoto wa asili ikiwemo kampeni ya upandaji wa miti katika maeneo mbalimbali ya nchi," amesema Maganga.

Kwa mujibu wa Bi. Maganga amesema kuwa inakadiriwa duniani kote takribani ekari milioni 18.7 za misitu hupotea kila mwaka kutokana na umuhimu wa urejeshaji wa ardhi, Tanzania imetenga ukubwa wa eneo takriban asilimia 40 ya eneo lote la ardhi ikijumuisha 6.5% ya bahari na 33% ya maeneo ya nchi kavu.

Maganga amesema katika kuunga mkono juhudi za kidunia za urejeshaji wa ardhi na uhifadhi wa mazingira, Tanzania imezindua Sera ya Taifa ya Mazingira (2022) na Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032) ambao umezingatia mipango shirikishi ya usimamizi wa mazingira katika ngazi zote.

Amesema lengo la mradi huo wa TRI ni kuimarisha usimamizi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibika ili kuleta ustawi wa mifumo-ikolojia na jamii kwani ni sehemu ya mradi mkubwa wa kidunia unaotekelezwa katika nchi 11 duniani ikiwemo Tanzania

Awali Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Kemilembe Mutasa amesema warsha hiyo ya siku tano imekusudia kuwakutanisha wataalamu hao na kuweka mikakati ya pamoja ya utekelezaji wa miradi ya urejeshaji katika mataifa 10 duniani na kuanisha mbinu za upatikanaji wa rasilimali muhimu za usimamizi wa miradi hiyo.

"Warsha hii imeshirikisha wataalamu wanaotekeleza mradi wa TRI na kwa pamoja tutajengeana uwezo, mbinu na mikakati mbadala yenye uhalisia na nadharia ya kila nchi kutoka katika ukanda na namna inavyotekeleza na kusimamia miradi ya TRI" amesema Kemilembe.

Kwa upande wake Meneja Tathimi-



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akifungua warsha ya wadau wa mazingira kutoka mataifa 10 duniani yanayotekeleza Programu ya Urejeshaji ya kidunia (TRI) Novemba 6, 2023 Jijini Dar es Salaam.*



*Afisa Misitu Mwandamizi kutoka Shirika la Chakula Dunia (FAO) Bw. Benjamin De Ridder akizungumza jambo wakati wa ufunguzi wa warsha ya wadau wa mazingira kutoka mataifa 10 duniani yanayotekeleza Programu ya Urejeshaji ya kidunia (TRI) Novemba 6, 2023 Jijini Dar es Salaam. Wengine wa pili kulia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga, Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Kemilembe Mutasa, Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Mazingira (IUCN) kutoka makao makuu Geneva, Uswisi Bi. Carole Saint- Laurent na Meneja tathimini na ufuatiliaji wa miradi kutoka Shirika la Kimataifa la Dunia (IUCN) Dkt. Francis Musau.*



*Mkurugenzi Msaidizi Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Thomas Bwana (katikati) na Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai (SLR) Dkt. Damas Mapunda wakifuatilia kikao cha warsha ya wadau wa mazingira kutoka mataifa 10 duniani yanayotekeleza Programu ya Urejeshaji ya kidunia (TRI) Novemba 6, 2023 Jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Afisa Mazingira Mwandamizi Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Joseph Kiruki.*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (katikati) akiwa katika poicha ya pamoja na watendaji waandamizi kutoka Mashirika ya IUCN, FAO na UNEP muda mfupi baada ya kufungua warsha ya wadau wa mazingira kutoka mataifa 10 duniani yanayotekeleza Programu ya Urejeshaji ya kidunia (TRI) Novemba 6, 2023 Jijini Dar es Salaam.*

ni na Ufualitiaji wa Shirika la Kimataifa la Mazingira (IUCN) Tanzania Dkt. Francis Musau, ameishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa usimamizi na utekelezaji wa mradi wa urejeshaji na kuitaja kuwa ni miongoni mwa nchi ya mfano inayotekeleza vyema miradi hiyo ya TRI.

Naye Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai (SLR) kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Dkt. Damas Mapunda amesema malengo ya mradi huo ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa mazingira na urejeshaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo-ikolojia na jamii nchini.

Amesema mradi huo hapa nchini unatekelezwa katika katika Mikoa 5 Halamshauri 7, Kata 18 na Vijiji 54 ambapo eneo la mradi linajumuisha mifumo ikolojia ya mabonde matatu ya Ruaha Mkuu na Ziwa Rukwa.

Amezitaja Halmashauri zinazotekeleza mradi huo ni pamoja na Halmashauri za Wilaya za Iringa Vijijini (Iringa), Mbeya na Mbarali (Mbeya), Wanging'ombe (Njombe), Halmashauri za Sumbawanga vijijini (Rukwa), Tanganyika na Mpimbwe (Katavi).

Mradi wa SLR unaofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Nchi nyingine zinazotekeleza mradi huo ni pamoja na Cameroon, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, China, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Guinnea Bissau, Kenya, Myanmar, Pakistan, Sao Tome& Principe.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akifanya mazungumzo na Rais wa Slovenia Mhe. Natasa Pirc Musar Mazungumzo yaliofanyika katika Mji wa Doha nchini Qatar tarehe Machi 07, 2023.*

# Makamu wa Rais, Rais wa Slovenia wajadili ushirikiano hifadhi ya mazingira



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akimkabidhi zawadi Rais wa Slovenia Mhe. Natasa Pirc Musar mara baada ya Mazungumzo yao yaliyofanyika katika Mji wa Doha nchini Qatar tarehe Machi 07, 2023.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Slovenia Mhe. Natasa Pirc Musar katika Mji wa Doha nchini Qatar kando ya Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea (LDCs), tarehe Machi 7, 2023.

Viongozi hao wamejadiliana masuala mbalimbali ya ushirikiano katika sekta za kimaendeleo pamoja na uhifadhi wa mazingira ambapo Rais wa Slovenia ameikaribisha Tanzania kushirikiana katika kupata teknolojia rafiki kwa mazingira ambayo nchi hiyo imewekeza zaidi.

Mazungumzo hayo yamehudhuriwa na Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Saada Mkuya, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Mbarouk Nassoro Mbarouk pamoja na Naibu Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa (New York) Mhe. Balozi Dkt. Suleiman Haji Suleiman.

Makamu wa Rais alikuwa nchini Qatar kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea (LDC5) uliofanyika Machi 05 hadi 09, 2023.

# TABAKA LA OZONI:

# Mikakati ya Serikali kulilinda



*Mkufunzi kutoka Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) Bagamoyo Bw. Goodluck Rulagora akitoa mafunzo kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji wa kemikali nchini kwa Maafisa wa Idara za Serikali zilizopo katika Mpaka wa Horohoro, Tanga tarehe 11 hadi 12 Februari, 2023.*

Ozoni ni tabaka la hewa lililopo kwenye angahewa ya juu, takribani kilometa 15 hadi 30 juu ya ardhi likiwa na kazi ya kuchuja kiwango kikubwa cha mionzi ya jua isifike kwenye uso wa dunia.

Tabaka la ozoni linapoharibiwa huruhusu mionzi ya jua kufika kwenye uso wa dunia na hivyo kusababisha kuongezeka kwa magonjwa mbalimbali yakiwemo saratani ya ngozi, mtoto wa jicho, upungufu wa kinga dhidi ya maradhi na kujikunja kwa ngozi. Pia huathiri kwa ukuaji wa mimea.

Mwanzoni mwa miaka ya 1970, wanasayansi walibaini baadhi ya kemikali zinazotengenezwa na kutumika katika baadhi ya vifaa ikiwemo majokofu, viyoyozi, vifaa vya kuzimia moto na utengenezaji wa magodoro vimejipenyeza angani na kumong'onyoa tabaka la hewa ya Ozoni na kusababisha madhara kwa afya ya binadamu na mazingira.

Baadhi ya kemikali zinazotumika katika majokofu na viyoyozi, vifaa vya kuzimia moto, usafishaji chuma, utengenezaji magodoro, ufukizaji wa udongo katika vitalu vya tumbaku na kilimo cha maua pamoja na hifadhi ya nafaka katika maghala husababisha kuongezeka kwa joto duniani na hivyo kuchangia katika mabadiliko ya tabianchi.

Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) lilifanya tathmini ya kisayansi na kuchukua hatua madhubuti kulinda tabaka hilo kwa kuanzisha Itifaki ya Montreal kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni iliyopitishwa mwaka 1987.

Septemba 16, 2023, Tanzania iliungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya

# TABAKA LA OZONI:



*Mafundi wa majokofu na viyoyozi wa jijini Dodoma wakihudumia jokofu lililopata hitilafu ambapo wana jukumu la kuhifadhi tabaka la ozoni katika shughuli zao.*

Hifadhi ya Tabaka la Ozoni kama kumbukumbu ya tarehe ya kutiwa saini Itifaki hiyo.

Kaulimbiu ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni mwaka 2023 ilikuwa ni 'Hifadhi ya tabaka la ozoni na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi' ambayo imechaguliwa kutokana na mafanikio ya kimataifa kupitia utekelezaji wa Itifaki ya Montreal katika kuchangia jitihada za kuhifadhi tabaka la ozoni na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, mwaka 1996, Serikali iliandaa na kutekeleza Programu ya Taifa ya kuondosha matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni ili kuhakikisha kwamba hakuna sekta ya uchumi au jamii inaathirika kutokana na matakwa ya Itifaki ya Montreal.

Hivyo, programu hii ilianzisha utaratibu wa kusimamia na kudhibiti uingizaji wa kemikali na bidhaa zenye kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni kutoka nje ya nchi.

### Jitihada za Serikali katika kuhifadhi tabaka la ozoni

Chini ya Programu ya Taifa, Serikali imeandaa na inatekeleza Mpango wa Kuondosha Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni Jamii ya Hydrochlorofluorocarbons (HCFCs) ifikapo mwaka 2030.

Hali kadhalika chini ya mpango huu mojawapo ya shughuli zinazotelekezwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa maafisa forodha na wasimamizi wa Sheria nchini kuhusu utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira yaani Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni za mwaka 2022 na utekelezaji wa Mikataba ya Vienna na Montreal nchini.

Mwaka 2022 Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau iliadhimisha Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi tabaka la ozoni na kuhamasisha matumizi ya kemikali ambazo ni rafiki kwa mazingira.

Pia, ilitoa mafunzo kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji wa kemikali nchini kwa Maafisa wa Idara za Serikali zilizopo katika Mpaka

# TABAKA LA OZONI:

wa Namanga na kwa wanafunzi wa fani ya viyoyozi katika Chuo cha Ufundi Arusha pamoja na mafundi wa viyoyozi na majokofu kwa Mkoa wa Arusha kuhusu namna bora ya kukarabati vifaa hivyo pasipo kuachia angani kemikali na hivyo kuharibu mazingira.

Pia, Maafisa Forodha na Wasimamizi wa Sheria waliopo katika Bandari ya Dar es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere walipatiwa mafunzo kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji wa kemikali na vifaa vyenye kemikali zinazodhibitiwa na Itifaki.

### Kauli ya Serikali

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo anatoa rai kwa kila mwananchi kushiriki katika kuhifadhi tabaka la ozoni na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Anasisitiza kuepuka kuingiza nchini gesi zilizopigwa marufuku na vifaa vinavyotumia gesi haribifu kama vile majokofu na viyoyozi vilivyokwishatumika (mitumba).

Hivyo, kwa muktadha huo Dkt. Jafo anaiasa jamii kununua bidhaa zilizowekwa nembo rasmi isemayo 'Ozone friendly' au 'low global warming potential' au 'sahibu wa ozoni' au 'uwezo mdogo wa kuchangia ongezeko la joto duniani'.

Pamoja na hayo pia wananchi wanaaswa kuepuka kutupa ovyo majokofu ya zamani ama vifaa vya kuzima moto vyenye kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni au kusababisha ongezeko la joto duniani.

### Mafundi wanufaika wa mafunzo

Charles Simon na Jairus Simon ambao wanajishughulisha na ufundi wa majokofu na viyoyozi jijini Dodoma kwa pamoja wanaishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuwapatia mafunzo.

Wanasema kuwa awali walikuwa hawana uelewa kuhusu athari zinazoweza kutokea katika tabaka la ozoni pindi gesi zisizotakiwa zinapoachiwa kusambaa angani.

Mafundi hao wanaeleza kuwa Serikali imewajengea uwezo wa namna bora ya kukarabati vifaa hivyo kwa umakini bila kuachia angani kemikali na hivyo kuharibu mazingira hususan tabaka la ozoni.

### Mafunzo kwa Wanahabari

Itakumbukwa Septemba 16, 2023 Serikali kupitia Ofisi ya Makamu ilitoa elimu kwa Chama cha Wanahabari wa Mazingira Tanzania (JET) na Wahariri kutokana na mchango wao mkubwa katika kufikisha elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Abdallah Hassan Mitawi anawahakikishia wanahabari kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari katika kuhakikisha elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira inaifikia jamii.

> Naiasa jamii kununua bidhaa zilizowekwa nembo rasmi isemayo 'Ozone friendly' au 'low global warming potential' au 'sahibu wa ozoni' au 'uwezo mdogo wa kuchangia ongezeko la joto duniani.' - **Dkt. Jafo**

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Mariam Mziwanda anaishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutambua mchango wa vyombo vya habari katika kutoa elimu kuhusu udhibiti wa tabaka la ozoni katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Anasema suala la usimamizi wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira halipaswi kuachiwa Serikali pekee hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuunga mkono juhudi hizo.

### Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) ni mojawapo ya taasisi za Serikali ambao ni wadau wakubwa wa usimamizi wa kemikali zinazoingia nchini.

Mojawapo ya majukumu iliyopewa ni pamoja na ubatilishaji na kutoa maelekezo au uteketezaji wa vitu, kemikali na mazao ya kemikali.

Meneja wa Kanda ya Kati wa GCLA, Gerald Meliyo anatoa wito kwa jamii hususan waingizaji wa kemikali nchini kufuata sheria kwa kuingiza kemikali zisizoharibu tabala la ozoni au zinazoongeza joto duniani.

Aidha, anatoa rai kwa wananchi kabla ya kununua bidhaa zenye kemikali wawe makini na kusoma nembo ili kutambua kama zimeruhusiwa kutumika ama la hatua itakayosaidia katika kulinda mazingira.

Meliyo anawaonya wanaoingiza mitungi ya gesi iliyoandikwa kwa lugha isiyokuwa ya Kiswahili au Kiingereza na iwapo watabainika watachukuliwa hatua kali ikiwemo bidhaa hizo kuteketezwa kwa gharama zao.

Ni wajibu wa kila mwananchi kulinda na kuhifadhi tabaka la ozoni na mazingira kwa ujumla kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeokoa uhai wa vizazi vya sasa na vijavyo.

# Makamu wa Rais achagiza upandaji miti kuadhimisha Mapinduzi ya Zanzibar



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akizungumza mara baada ya zoezi la upandaji miti lililofanyika katika eneo la Ihumwa na Msalato jijini Dodoma wakati wa Maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tarehe 12 Januari 2023.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ameongoza zoezi la upandaji miti katika maeneo ya Ihumwa na Msalato jijini Dodoma tarehe 12 Januari, 2023 ikiwa ni katika kusheherekea maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Akizungumza na viongozi na wananchi Mhe. Dkt. Mpango amesema suala la upandaji miti linapaswa kuwa la lazima na kuziagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha wanafikia lengo la upandaji miti milioni moja na laki tano kwa mwaka kama ilivyopangwa.

Amesisitiza ushirikishwaji wa sekta binafsi na wafanyabiashara katika upandaji na utunzaji miti pamoja na kuzisihi familia kuongeza juhudi katika upandaji miti na usafi wa mazingira. Amezitaka taasisi za Serikali kupanda miti katika maeneo yao na kuhakikisha inastawi.

Makamu wa Rais amewataka viongozi kuwa mfano katika zoezi la upandaji na utunzaji miti kwa kuonesha kwa vitendo ambapo ameagiza Jiji la Dodoma kuratibu zoezi la usimamiaji miti ilioyopandwa ili kuhakikisha inaishi na kupendezesha jiji.

Aidha amewataka kudhibiti masuala yote ya uchomaji moto maeneo yaliopandwa miti pamoja kukabiliana na changamoto ya uingizaji au upitishaji mifugo katika maeneo hayo.

Pamoja na hayo Mhe. Dkt. Mpango amesema kila mwananchi anapaswa kuimwagilia miti iliopandwa mbele yake hususani wale wanaomiliki vituo vya mafuta na wanaozalisha tofali.

Ametoa wito kwa waandishi wa habari nchini kutoa kipaumbele katika kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya upandaji miti na uhifadhi wa mazingira kwa ujumla.

"Ni muhimu kwa waandishi wa habari kutoa habari za mifano ya wale walioweza kutunza mazingira ili wawe hamasa kwa watanzania wengine," amesisitiza Makamu wa Rais.

Katika hatua nyingine, Mhe. Dkt.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akipanda mti aina ya Mdodoma kandokando ya Barabara ya Dodoma – Morogoro eneo la Ihumwa jijini Dodoma wakati akiongoza zoezi la upandaji miti kuadhimisha Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tarehe 12 Januari 2023.*

Mpango ameagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kupitia upya utaratibu wa leseni za ukataji miti kwa ajili ya mkaa ili kuokoa maeneo ambayo yana uoto na vyanzo vya maji.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amesema tayari mipango mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira imeanza kutekelezwa. Amefafanua kuwa tayari maeneo yaliopandwa miti yamegawiwa kwa taasisi za Serikali na za binafsi ili waweze kusimamia na kuhakikisha kuwa miti hiyo inastawi na kuishi.

Kutokana na hatua hiyo, Waziri Dkt. Jafo amemuhakikishia Makamu wa Rais kuwa zoezi la upandaji miti na kuitunza litakuwa endelevu wakati wote.

Kwa upande wake Mdau wa Mazingira na Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda ametoa wito kwa wananchi kuzingatia utaratibu wakati wa upandaji wa miti ikiwemo kuandaa mazingira ya upandaji na kufuata maelekezo ya wataalamu ili kufahamu aina ya mti na mahali unapopaswa kupandwa.

Mhe. Pinda amesema Jiji la Dodoma linakabiliwa na upungufu wa mvua hivyo, ni vyema uchimbaji wa mashimo pamoja na nafasi baina ya mti na mti ukawa wa kitaalamu zaidi ili kuepusha miti hiyo kutofikia lengo.

Pia Mhe. Pinda amesema Jamii inao wajibu mkubwa wa kusimamia na kutekeleza kwa makini yale yote yanayopelekea Maisha ya binadamu kuwa salama ikiwemo upandaji wa miti na kuhakikisha inafikia lengo.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amesema upandaji miti katika vyanzo vya maji umepewa kipaumbele mkoani Dodoma kwa kuanza na Bonde la Mzakwe ambalo limekuwa na changamoto ya ukuaji wa miti.

Mhe. Senyamule amesema tayari wataalamu wamewezesha aina ya miti inayopaswa kupanda pamoja na kuweka mazingira yatakayookoa miti hiyo dhidi ya hatari ya moto.

# Makamu wa Rais aifungulia milango Qatar kuwekeza katika teknolojia kukabili mabadiliko ya tabianchi



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akifanya mazungumzo na Balozi wa Qatar nchini Tanzania Mhe.Fahad Rashid Al-Muraikhi, mazungumzo yaliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma Oktoba 23, 2023.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akiagana na Balozi wa Qatar nchini Tanzania Mhe. Fahad Rashid Al-Muraikhi mara baada ya mazungumzo yaliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma Oktoba 23, 2023.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ameikaribisha Qatar kushirikiana na Tanzania katika teknolojia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo kuwasaidia wananchi kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa na kuimarisha matumizi ya nishati mbadala.

Pia amesema Qatar na Tanzania zinaweza kushirikiana kwenye utalii pamoja na uwekezaji katika rasilimali watu ikiwemo wataalamu wa afya pamoja na uwekezaji katika viwanda vya uzalishaji dawa na vifaa tiba pamoja

Makamu wa Rais amesema hayo wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Qatar nchini Tanzania Mhe.Fahad Rashid Al-Muraikhi, Oktoba 23, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Amesema Tanzania inathamini ushirikiano uliopo baina yake na Qatar na imedhamiria kuimarisha na kuendeleza ushirikiano huo kwa manufaa ya mataifa yote mawili.


Aidha, Mhe. Dkt. Mpango ametaja maeneo yanayoweza kuongezwa ushirikiano baina ya Tanzania na Qatar ikiwemo sekta ya afya, utafiti wa mafuta na gesi pamoja na biashara ikiwemo bidhaa zinazotokana na mafuta.

Kwa upande wake Balozi wa Qatar nchini Tanzania Mhe. Al-Muraikhi amesema Tanzania na Qatar zinapaswa kuongeza ushirikiano wake ili kuweza kutumia vema fursa zilizopo katika mataifa hayo.


Hali kadhalika Balozi huyo ameahidi kufanya kazi kwa karibu na Serikali ya Tanzania ili kuongeza ushirikiano katika masuala ya kibiashara.

Kwa pamoja viongozi hao wamejadili namna ya kufanyika kwa ziara za wafanyabiashara na wawekezaji baina ya mataifa hayo mawili ambazo zitaweza kusaidia kuimarisha ushirikiano katika sekta mbalimbali ikiwemo za afya, michezo na utamaduni.

# MAKAMU WA RAIS ASHIRIKI MKUTANO WA SADC KWA NJIA YA MTANDAO








*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amemwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) uliofanyika kwa njia ya mtandao Oktoba 31, 2023 jijini Dodoma.*




# Dkt. Mpango: Taasisi za fedha ziwezeshe viwanda vidogo kukuza uzalishaji

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa Taasisi za fedha nchini kuweka masharti ya mikopo ya upendeleo kwa viwanda vidogo na vya kati ili kukuza uzalishaji na kuimarisha sekta hiyo.

Makamu wa Rais ametoa wito huo wakati wa kilele cha Maonesho ya Nne ya Kitaifa ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) yaliyofanyika katika Uwanja wa Sabasaba mkoani Njombe Oktoba 28, 2023.

Mhe. Dkt. Mpango amesema kuwa ni muhimu kushughulikia suala la upatikanaji wa mitaji kwa riba nafuu ili kuwawezesha wajasiriamali kuweza kuanzisha viwanda vidogo na vya kati.

Amesema katika kuongeza thamani ya bidhaa na mazao, suala la vifungashio lina umuhimu mkubwa hivyo SIDO na taasisi nyingine katika tasnia ya viwanda vidogo vidogo inayo nafasi ya kutoa mchango katika kubuni na kuhamasisha uzalishaji wa vifungashio bora na vyenye viwango kwa kutumia teknolojia rahisi na na-

fuu. Pia, Makamu wa Rais amesema kuwa tafiti zina umuhimu mkubwa katika kukuza matumizi ya teknolojia mbalimbali kwenye uzalishaji na uongezaji thamani wa bidhaa na mazao.

Ameitaka SIDO kuanza kujiendesha kibiashara pamoja na kuanzisha tuzo kwa wabunifu wa mashine na wazalishaji bora wa bidhaa kutoka viwanda vidogo vidogo katika mfumo wa fedha, vyeti au mafunzo maalum kwa wajasiriamali waliofanya vizuri zaidi.

Pia Mhe. Dkt. Mpango ameliagiza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kufanya jitihada zaidi kuwafikia wajasiriamali wadogo kupata uthibitisho wa ubora wa bidhaa zao kwa gharama nafuu.

Amesema dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kujenga uchumi shindani wa viwanda ili kuifikisha nchi kwenye kipato cha kati cha juu na kwamba maonesho hayo yamesaidia kuibua masuala kadhaa yanayoathiri maendeleo ya viwanda vidogo vidogo.

Katika hatua nyingine Makamu wa Rais amesema Serikali imedhamiria kujenga uwanja mpya wa ndege wenye urefu wa kilomita tatu utakaowezesha ndege kubwa za abiria na mizigo kutua pamoja na ujenzi wa jengo la abiria na jengo maalum la kuhifadhia bidhaa zinazoharibika haraka (cold room) katika mkoa wa Njombe.

Pia amesema Wizara ya Elimu inatambua umuhimu wa ujenzi wa Chuo Kikuu katika mkoa huo na kwa hatua za awali taratibu za kuanzisha Kampasi ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) zinaendelea kufanyika na zitakapokamilika ujenzi utaanza mara moja.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe amesema wizara hiyo inaendelea kupitia na kufanya marejeo ya sera na sheria mbalimbali za taasisi ikiwemo sheria iliyounda SIDO ili kuendana na hali ya sasa ambayo italiwezesha shirika hilo kutoa huduma zenye tija na ushindani.

Ameongeza kwamba Serikali imewezesha upatikanaji wa fedha ambazo zimesaidia SIDO kuboresha miundombinu yake ikiwemo kuboresha vituo sita vya uendelezaji wa teknolojia na ubunifu kwa kuweka mitambo ya kisasa yenye thamani ya shilingi bilioni 1.65 katika mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro, Iringa, Shinyanga, Lindi na Kigoma. Pia kuongeza mtaji wa shilingi bilioni 1.69 kwenye mfuko wa kukopesha wajasiriamali (NEDF).

Awali akitoa taarifa za maonesho hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Sido Mhandisi Mussa Nyamsingwa amesema maonesho hayo yanalenga kuwawezesha wananchi kufahamu huduma zinazotolewa na SIDO na bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali kwa manufaa yao na Taifa kwa ujumla.

Aidha amesema maonesho hayo yamekuwa yakichochea ukuaji wa ajira, kutekeleza shughuli za kiuchumi katika sekta mbalimbali hasa katika uongezaji wa thamani wa mazao pamoja na kuchochea ubunifu na uzalishaji wenye tija.

Maonesho hayo yenye kaulimbiu isemayo "Pamoja Tujenge Viwanda Kwa Uchumi na Ajira Endelevu" yalianza tarehe 21/10/2023 ambapo yameshirikisha wajasiriamali wapatao 805, Teknolojia 95 zinazotumika katika Minyororo 22 ya thamani ya mazao na Taasisi 30 za Serikali na Binafsi.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akitembelea mabanda mbalimbali katika Maonesho ya Nne ya SIDO Kitaifa yanayofanyika uwanja wa Sabasaba mkoani Njombe.*

# GEF yaridhishwa na utekelezaji wa Mradi wa EBARR Mpwapwa

Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) umeridhishwa na utekelezaji wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia vijijini (EBARR) unaotekelezwa katika Wilaya ya Mpwapwa Mkoani Dodoma na kusimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Hayo yamesemwa na Mratibu wa GEF Kanda ya Afrika Dkt. Ibrahima Sow wakati wa ziara ya kutembelea Mradi huo katika vijiji vinne vya wilaya hiyo, tarehe 15 Februari, 2023.

Dkt. Sow amesema GEF imeridhirishwa na utekelezaji wa miradi hiyo ambayo ni ujenzi wa visima virefu vinne, malambo mawili, majosho mawili, vitalu nyumba vitatu na mashine ya kukamulia alizeti ambapo miradi hiyo imeweza kuwa chanzo mbadala cha kuongeza kipato kwa wananchi.

> Miradi hii ina faida kubwa kwa wananchi wa Mpwapwa, natoa rai kwa jamii kuitunza na kuwasaidia kwa ajili ya kuleta manufaa ya sasa na kwa kizazi kijacho

"Miradi hii ina faida kubwa kwa wananchi wa Mpwapwa, natoa rai kwa jamii kuitunza na kuwasaidia kwa ajili ya kuleta manufaa ya sasa na kwa kizazi kijacho" amesema Dkt. Sow ambaye aliambatana na Ujumbe kutoka Sekretarieti ya GEF.

Sow amesema GEF itaendelea kufadhili miradi ya mazingira inayozunguka jamii ili kuongeza kasi ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika maeneo ya vijijini sambamba na kuhakikisha jamii inajishughulisha na kilimo rafiki kwa mazingira na kutolea mfano kilimo cha mbogamboga.

Kwa upande wake Mratibu wa Mradi wa EBBAR Kitaifa, Dkt. Makuru Nyarobi amewataka wananchi wa wilaya hiyo kusimamia vyema miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao ambayo inatarajia kuwanufaika wananchi wa vijiji vya Ng'hambi, Mbugani, Kiegea na Kazania.



*Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia (EBARR) Dkt. Makuru Nyarobi akitoa ufafanuzi kwa Ujumbe wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) ukiongozwa na Mratibu wa Kanda ya Afrika, Dkt. Ibrahima Sow wakati wa ziara ya kutembelea mradi huo Februari 15, 2023.*

Ameongeza kuwa Mradi huo pia unatekelezwa katika wilaya nyingine nne ambazo ni Kaskazini 'A' Unguja (Zanzibar), Simanjiro (Manyara), Mvomero (Morogoro) na Kishapu (Shinyanga) na kueleza kuwa miradi hiyo imetekelezwa kwa kutumia mifumo ikolojia ambapo mipango ya matumizi ya ardhi imeandaliwa.

Kwa upande wake Mtendaji wa Kijiji cha Mbugani, Aziza Mwinyimbweni amesema Serikali ya Kijiji hicho imejipanga katika kuhakikisha kuwa mradi huo unafikia malengo yaliyowekwa na Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii ikiwemo maji safi na salama.

Ujumbe wa GEF ulikuwa jijini Dodoma tarehe 13 hadi 14 Februari, 2023 na kuendesha warsha kwa wadau na wataalamu wa mazingira kutoka Serikali Kuu, TAMISEMI, Wakala, Idara na Wakala za Umma na sekta binafsi kwa ajili ya kuibua vipaumbele vya miradi ya mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi.



*Afisa Mazingira Mwandamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) Bw. Filippo Berarch akitazama mbegu za alizeti zinazotumika kwa ajili ya kutengeneza mafuta na mashudu ya vyakula vya mifugo wakati wa ziara ya ujumbe huo kukagua Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR) Februari 15, 2023 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma.*



*Ujumbe wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) ukiangalia mashine ya kukamua mafuta ya alizeti wakati wa ziara ya kukagua Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR) Februari 15, 2023 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma.*




# Pimeni maeneo ya malisho ya mifugo ili kupunguza migogoro – Waziri Jafo

Serikali imeelekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ipime maeneo ya malisho ya mifugo ili kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Maelekezo hayo yametolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo wakati akifunga Wiki ya Maonesho ya Ufugaji wenye Tija na Utunzaji wa Mazingira kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Biteko jijini Dodoma, Novemba 3, 2023.

Amesema wizara hiyo ishirikiane na TAMISEMI na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kutenga maeneo ambayo yatatumiwa na wafugaji katika kulisha mifugo yao kwa utaratibu hivyo kuepuka na uharibifu wa mazingira.

Pia, Waziri Jafo ameitaka Wizara ya Maji kupitia Mamlaka za Mabonde nchini kuhakikisha yanalindwa sanjari na kusimamia zoezi la upandaji wa miti katika vyanzo vya maji ili yawasaidie wakulima na wafugaji.

"Vyuo vikuu vya kilimo na mifugo viendeleze tafiti mbalimbali za kuangalia aina ya malisho ambayo yatawasaidia wafugaji wetu kupata malisho ya uhakika kwa ajili ya mifugo," amesema Dkt. Jafo.

Aidha, Waziri amekipongeza Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija Tanzania (CHAMAUTA) kwa kusajili wafugaji nchini na kuwataka kuendelea na zoezi hilo ambalo litasaidia katika kuweka mfumo mzuri wa utunzaji wa mazingira.

Dkt. Jafo ambaye pia ni mlezi wa chama hicho amewapongeza kwa kuweka kipaumbele agenda ya mazingira na kusema Serikali itaendelea kuwaunga mkono.

Amewaomba wafugaji waendelee kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amejipambanua katika uhifadhi wa mazingira hususan kupitia miradi mikubwa anayotekeleza ikiwemo inayowagusa wafugaji.

Akifungua maonesho hayo na kuzindua chama hicho, Waziri Jafo amewataka wafugaji kuwa mabalozi wa uhifadhi mazingira kwa kufanya ufugaji wa kimkakati na endelevu.

Aidha, Waziri Dkt. Jafo amesema kuwa ufugaji endelevu usioathiri hifadhi ya mazingira utasaidia katika kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji inayotokea katika baadhi ya maneo nchini. Hali kadhalika Waziri Jafo ametoa wito kwa CHAMAUTA kulitumia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupata uelewa kuhusu kanuni na zinazosimamia mazingira ili kuepuka shughuli zinazoharibu mazingira.

Amewataka wafugaji nchini kuunga mkono juhudi za Serikali chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye anaendelea kuiletea nchi maendeleo ikiwemo kuendeleza sekta ya maji.

Amesema kupitia miradi mbalimbali Serikali imekuwa ikichimba malambo kwa ajili ya kunyweshea mifugo hususan katika maeneo yenye ukame hatua inayosaidia

Kwa upande wa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Mhe. Remidius Mwema aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ameipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kusimamia utekelezaji wa uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Amesema kuwa mikakati ya kuhifadhi vyanzo vya maji katika eneo la Makutupora inaendelea na kuwa tayari chanzo hicho kimeanza kutoa asilimia 61 ya mahitaji ya maji kwa mkoa.

Aidha, Mhe. Mwema amesema kuwa Serikali ya Mkoa inaendelea na Kampeni ya Kukijanisha Dodoma ambapo inaendelea kuandaa vitalu vya miche ili kukabiliana na upungufu wa miche.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akimkabidhi nakala ya mwongozo wa Ukaguzi wa Mazingira kwa Miradi ya Ujenzi wa Majengo aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Samuel Gwamaka baada ya uzinduzi wa mwongozo huo jijini Dodoma Oktoba 18, 2023. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NEMC Mhandisi Prof. Esnati Chaggu.*

# Dkt. Jafo azindua Mwongozo ukaguzi wa mazingira miradi ya ujenzi

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amezindua Mwongozo wa Ukaguzi wa Mazingira kwa Miradi ya Ujenzi wa Majengo Oktoba 18, 2023 jijini Dodoma.

Mwongozo huo umeandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC kwa kushirikiana na Kituo cha Sayansi na Mazingira cha nchini India (CSE).

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi, Waziri Dkt. Jafo ameitaka NEMC kuongeza wigo wa kuandaa miongozo ya Tathimini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kupitia sekta za viwanda, nishati, kilimo na maji ili kuharakisha zoezi la mapitio ya miradi ya tathimini za athari kwa mazingira.

Amesisitiza kuwa uhifadhi na usimamizi wa mazingira ni mojawapo ya maeneo ya vipaumbele vilivyopo katika malengo makuu ya Serikali hivyo mwongozo huo umezingatia mahitaji halisi ya nchi ikiwemo ukuaji wa miji na majiji. Hivyo, amesema NEMC imepewa mamlaka ya kuhakikisha hali ya mazingira inaboreshwa nchini kwa kusaidia uboreshaji wa afya ya jamii ikiwa ni pamoja na mazingira vinalindwa na kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini.

"Kipengele namba. 17 cha Makubaliano ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu unazitaka nchi wanachama kuhusisha tathmini za athari za mazingira katika miradi ambayo inasababisha madhara kimazingira....katika kutekeleza kipengele hicho zilianzisha taasisi, na kutengeneza Sera na Sheria ikiwa ni pamoja na Kanuni kama ilivyo kwenye Kanuni ya Athari ya Mazingira za Mwaka 2005 na zile za Mwaka 2018," amesema Dkt. Jafo.

Amefafanua kuwa sema TAM hufanyika ili kuweka mifumo bora ya kulinda mazingira ikiwa ni pamoja na kupunguza kiwango cha taka zinazozalishwa, kutoa kipaumbele katika masuala ya jamii, kuainisha athari zilizopo na madhara yanayoweza jitokeza kutokana na miradi inayoanzishwa.

Waziri Jafo amesema NEMC inapokea zaidi ya miradi 2,000 kwa mwaka kwa ajili ya mapitio na kuongeza kuwa idadi hiyo ya miradi ni kubwa na itaweza kupitiwa kwa ufanisi iwapo kutakuwa na miongozo ya kila sekta kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

Ameishukuru Serikali ya India kupitia kituo hicho kwa kushirikiana na Baraza hilo kwa kuandaa mwongozo huo kwani ushirikiano huo ni ishara ya ya matokeo ya ushIrikiano wa taasisi hizo katika kupatia ufumbuzi wa changamoto za kimazingira.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa CSE, Bw. Nivit Yadav amesema Tanzania ni nchi ya tatu katika Bara la Afrika yenye kasi kubwa ya idadi ya watu na nchi ya pili kwa mataifa ya Afrika Mashariki kuwa na kasi ya ukuaji wa sekta ya ujenzi, hivyo suala la tathmini ya miradi ya ujenzi ni jambo muhimu linalopaswa kupewa kipaumbele katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Bw. Yadav amesema Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 imeanisha vipaumbele mbalimbali vya utekelezaji wa Sheria hiyo ikiwemo kanuni na miongozo ya utekelezaji ikiwemo ushirikiano baina ya Serikali kupitia NEMC na CSE.

Kwa upande wake aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu NEMC Dkt. Samwel Gwamaka amesema kwa muda mrefu kumekuwepo na changamoto ya usimamizi wa tathmini ya athari kwa mazingira kupitia maandiko ya miradi mbalimbali yanayowasilishwa kwa ajili ya utoaji wa vibali vya mazingira.

"Awali wataalamu wetu hawakuwa na mwongozo wa maandiko ya tathmini ya miradi ya athari za mazingira ambayo inakidhi matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kanuni zake....Baada ya uzinduzi huu sasa wataalamu elekezi wa mazingira na wadau watakuwa na mwongozo wa uaandaji wa maandiko kwa kuzingatia viwango na ubora unaohitajika," amesema Dkt. Gwamaka.

# Dkt. Jafo: Mkutano wa Wakuu wa Nchi EAC umeakisi sekta ya mazingira





*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo (kulia) akijumuika na Mawaziri wengine wa Serikali ya Tanzania kuimba wimbo wa Afrika Mashariki wakati wa Mkutano wa Kawaida wa 44 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika katika ukumbi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) jijini Arusha Novemba 22, 2023.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo ameshiriki Mkutano wa Kawaida wa 23 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) Ngurdoto mkoani Arusha Novemba 24, 2023.

Akizungumza mara baada ya kushiriki mkutano huo Dkt. Jafo amesema kuwa majadiliano yameakisi maeneo muhimu katika sekta ya mazingira hususan mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula.

Amesema Tanzania imekuwa ya mfano barani Afrika kwa kuchukua hatua muhimu za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia Serikali ya Awamu ya Sita.

Waziri Jafo amesema kuwa kazi kubwa imeonekana kwa upande wa mazingira kwa utekelezaji wa miradi ya mbalimbali ambayo kwa namna moja ama nyingine inawasaidia wananchi.

"Yamefanyika mapinduzi makubwa kupitia Serikali hususan katika sekta ya kilimo cha kisasa zaidi cha umwagiliaji, mradi wa reli ya kisasa na mabasi ya mwendo kasi yote hii imelenga kupunguza uchafuzi," amesema.

Mkutano huo ulipokea na kuridhia kwa kauli moja mapendekezo ya Majadiliano ya Juu kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Usalama wa Chakula yaliyofanyika Novemba 23, 2023 ambayo ni hatua ya kuifanya EAC kuwa na msimamo mmoja katika Mkutano wa COP28 uliofanyika Dubai, Falme za Kiarabu kuanzia Novemba 30 hadi Desemba 12, 2023.

Aidha, mkutano huo umeridhia ombi la Shirikisho la Jamhuri ya Somalia chini ya Rais Mhe. Hassan Sheikh Mahmoud kujiunga na EAC hiyo na kufanya jumla ya nchi wanachama wa jumuiya hiyo kuwa nane.

Mkutano huo umehudhuriwa na Rais wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Burundi Mhe. Evariste Ndayishimiye ambaye amemaliza muda wake wa Mwenyekiti na kumkabidhi kijiti Rais wa Sudan Kusini Mhe. Salva Kiir, Rais wa Kenya Mhe. William Ruto na Rais wa Uganda Yoweri Museveni.

Viongozi wengine ni Waziri Mkuu wa Rwanda Mhe. Dkt Edouard Ngirente aliyemwakilisha Rais Paul Kagame na Makamu Rais na Waziri wa Ulinzi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) aliyemwakilisha Rais wa nchi hiyo Mhe. Antonie Tshisekedi.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo (wa tatu kushoto) akishiriki Mkutano wa Kawaida wa 23 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) Ngurdoto mkoani Arusha Novemba 24, 2023. Kulia kwake ni Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Angela Kairuki na kushoto kwake ni Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa Zanzibar Mhe. Shamata Shaame Khamis.*



# Dkt. Mpango: Tumuenzi Baba wa Taifa kwa kufanya kazi kwa bidii



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa Watanzania kumuenzi Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha Maisha pamoja na kuinua uchumi wa Taifa.

Amesema hayo wakati akizungumza kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Misa Maalum ya Kitaifa ya Kumuombea Baba wa Taifa iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Roho Mtakatifu – Babati mkoani Manyara, Oktoba 14, 2023.

Dkt. Mpango amewasihi viongozi na Watanzania kwa ujumla kumuenzi Baba wa Taifa kwa kuishi katika misingi ya kukemea rushwa, kupiga vita umasikini, kutojilimbikizia mali pamoja na kukemea matendo mabaya.

Makamu wa Rais amesema ni wajibu kwa Watanzania kumuenzi kwa kuishi maisha aliyoishi kiongozi huyo kwa kuwa alitumia elimu na vipaji vyake kwa faida ya wote, alithamini dhamana aliyopewa, alikuwa mnyenyekevu na mwenye kujisahihisha alipokosea.

Ameongeza kwamba Mwalimu Nyerere alikemea matendo mabaya yaliochochea mmomonyoko wa maadili, alikuwa mwanamazingira hodari na alipiga vita umaskini.

Aidha Makamu wa Rais amelishukuru Kanisa pamoja na taasisi zingine za kidini kwa ushirikiano wake na Serikali kwa kutoa huduma mbalimbali za kijamii kama vile elimu, afya, mazingira na mengineyo. Serikali itaendelea kushirikiana vema na kanisa katoliki pamoja na madhehebu yote ya dini katika kuwatumikia Watanzania huku akiwasihi viongozi wa dini kuendelea kuliombea Taifa amani na utulivu.

Misa Maalumu ya Kitaifa ya kumuombea Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere imeongozwa na Askofu wa Jimbo Katoliki la Mbulu Anthony Lagwen na kuhudhuriwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Viongozi mbalimbali pamoja na waumini kutoka maeneo mbalimbali nchini.

# Dkt. Jafo: Serikali imewekeza katika teknolojia ya kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amesema Serikali imewekeza katika teknolojia ya kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kupitia miradi ya mazingira inayotekelezwa nchini.

Dkt. Jafo amesema hayo alipochangia mjadala wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) unaofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam Septemba 08, 2023.

Ametoa wito kwa nchi zilizoendelea kuunga mkono juhudi hizo za Serikali kwa kufadhili miradi ya kilimo inayotekelezwa nchini ili pawepo na tija na uhakika wa chakula.

Kutokana na Makubaliano ya Paris kuhusu nchi zilizoendelea kuchangia fedha kwa mataifa yanayoendelelea katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Waziri Jafo alipendekeza kupitia fedha hizo pia pawe na mafungu maalumu ya kuwezesha kilimo cha kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, Waziri Jafo alisema ili kukabiliana na changamoto ya ukame unaosababishwa na uhaba wa mvua katika baadhi ya maeneo Serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 200 kwa ajili ya uchimbaji wa malambo 114 ya umwagiliaji.

"Tunafahamu sekta ya kilimo inaathirika sana kwa maana mvua hazitoshi hivyo miradi ya uhimili ni muhimu

> **Tunafahamu sekta ya kilimo inaathirika sana kwa maana mvua hazitoshi hivyo miradi ya adaptation ni muhimu sana kama nchi hizo zikiwekeza katika teknolojia ya kilimo**







sana kama nchi hizo zikiwekeza katika teknolojia ya kilimo. Tuipongeze Serikali inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuja na Mradi wa BBT kwa vijana na tunaona umeanza kutimiza ndoto za vijana," alisema.

Aidha, katika kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija pamoja na kuwepo kwa changamoto za kimazingira, Dkt. Jafo alisema Serikali inaimarisha uzalishaji wa nishati ikiwemo mradi wa Bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere na kusambaza umeme vijijini.

Alifafanua kuwa hatua ya usambazaji nishati vijiji itasaidia kuwavutia wawekezaji kufungua viwanda vya uchakataji wa mazao na hivyo kukuza uchumi kwa kuuza bidhaa zilizochakatwa badala ya mazao ghafi.

"Katika mkutano huu tumewataka wenzetu watimize wajibu wao kuchangia fedha za kusaidia nchi zinazoendelea katika miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi hasa kwenye Kilimo cha Kisasa (smart agriculture) badala ya kutegemea," alisisitiza Waziri Jafo.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Japan Mhe. Yasushi Misawa pamoja na viongozi wengine mara baada ya mazungumzo yao yaliyofanyika Septemba 14, 2023 katika Mji wa Serikali, Mtumba Jijini Dodoma.*

# Tanzania, Japan zateta ufadhili miradi ya mazingira

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Japan hapa nchini, Mhe. Yasushi Misawa katika Mji wa Serikali, Mtumba Jijini Dodoma.

Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika leo Septemba 14, 2023 Dkt. Jafo amemshukuru Balozi Misawa kwa juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo (JICA) kwa kuendelea kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo maji, elimu, barabara, afya na kuiomba Serikali hiyo kusaidia pia miradi ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira iliyopo nchini.

Waziri Jafo amemueleza Balozi Misawa kuwa ajenda ya mazingira ni moja ya kipaumbele muhimu vilivyopewa msukumo na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea na juhudi za kuhamasisha jamii kutumia nishati mbadala ili kuhamasisha uhifadhi na utunzaji mazingira nchini.

"Tanzania tunazalisha takribani tani Milioni moja za taka ngumu ambazo ni fursa ya uzalishaji wa nishati mbadala...tunatumia asilimia 30 tu ya nishati hiyo...Tunahitaji nishati hii kwa ajili ya matumizi ya kijamii na kiuchumi. Tunahitaji wawekezaji wengi zaidi kujitokeza kwa ajili ya uwekezaji," amesema Mhe. Dkt.Jafo.

Amesema kuwa Serikali imeweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wawekezaji na wadau wa nishati hiyo kuweza kujitokeza na kushirikiana na Serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati mbadala hususani katika maeneo ya vijijini ili kuongeza upatikanaji wa nishati mbadala ya kupikia.

Waziri Jafo pia amemhakikishia Balozi Misawa ushirikiano na utayari wa Serikali ya Tanzania katika kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya nishati jadidifu ikiwemo jotoardhi, tungamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya Nishati mbadala ili kuleta manufaa kwa wananchi na jamii kwa ujumla.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingir) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akimkabidhi nyaraka mbalimbali za taarifa kuhusu majukumu ya Ofisi hiyo Balozi wa Japan nchini Tanzania Mhe. Yasushi Misawa mara baada ya mazungumzo baina yao yaliyofanyika Septemba 14, 2023 katika Mji wa Serikali, Mtumba Jijini Dodoma.*

Akifafanua zaidi Waziri Jafo amesema Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa sera, kanuni na miongozo mbalimbali ikiwemo ikiwemo katazo Kwa taasisi zote za umma na binafsi kwa upande wa Tanzania Bara zinazoandaa chakula na kulisha watu zaidi 300 kusitisha matumizi ya mkaa na mkaa ifikapo mwaka Januari 2025.

Dkt. Jafo amesema kutokana na msisitizo huo, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imendelea kuwahimiza wadau na washirika wa maendeleo kujitokeza kuungana mkono juhudi hizo za serikali kwa kuhakikisha zinaelekeza nguvu katika uwekezaji wa miradi ya nishati Rafiki kwa mazingira.

Aidha kwa upande mwingine Dkt. Jafo ameiomba Serikali ya Japan kutoa fursa ya ufadhili wa masomo kwa wataalamu wa mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais ili kuweza kujengewa uwezo wa kitaalamu na kiufundi katika usimamizi wa miradi mbalimbali ya mazingira inayotekelezwa nchini.

Kwa upande wake, Balozi Misawa amemhakikishia Waziri Jafo kuwa Serikali ya Japan itaendelea kuwa mdau mkubwa wa maendeleo kwa kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza sekta ya Nishati hasa kwa upande wa Nishati jadidifu.

Alisema, kuwa wawekezaji kutoka Japan wapo tayari kuja kuwekeza nchini Tanzania katika sekta ya nishati jadidifu na kuhakiikisha kuwa uwekezaji huo unaleta manufaa ya kijamii na kiuchumi baina ya Mataifa hayo.

# Zanzibar kunufaika na Biashara ya Kaboni



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis amesema Zanzibar inatarajia kunufaika na Biashara ya Kaboni wakati wowote kuanza sasa.

Amesema hayo Juni 13, 2023 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu maswali ya Mbunge wa Viti Maalumu Mhe. Maryam Azan Mwinyi.

> Ili kutekeleza suala hilo, wataalamu wapo katika hatua za mwisho za kufanya utafiti kwenye maeneo yenye misitu ya asili upande wa Tanzania Zanzibar

Mhe. Khamis amesema ili kutekeleza suala hilo, watalamu wapo katika hatua za mwisho za kufanya utafiti kwenye maeneo yenye misitu ya asili upande wa Tanzania Zanzibar.

Ameitaja Msitu wa Jozani uliopo Unguja na Ngezi katika Kisiwa cha Pemba kuwa inaweza kutumika kuvuna hewa ya ukaa na kuwapatia faida wananchi wa visiwani humo.

Kuhusu kuwapa uelewa wananchi, Naibu Waziri amebainisha kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar inatarajia kutoa elimu kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

"Mheshimiwa Naibu Spika utakumbuka pia juzi tumetoa semina kwa wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge za Maji na Mazingira pamoja na ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu hewa ya ukaa ili kuwanjengea uelewa," amesisitiza.

Amesema kuwa Serikali imeunda kikosi kazi kilichoshirikisha Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ambacho kinazunguka nchi nzima kutoa elimu kuhusu Biashara ya Kaboni husussan katika mikoa ya Tabora, Simiyu, Katavi na Manyara na maeneo mengine.

Hivyo, amesema kuwa Serikali imeweka mipango thabiti ya kusimamia na kutathmini biashara hiyo ambapo imetoa mamlaka kwa Kituo cha Kitaifa cha Kufuatilia Kaboni (NCMC) kilichopo mjini Morogoro ambacho kinaratibu na kutoa utaalamu kuhusu gesijoto nchini.

Sambamba na hilo pia imeandaa Kanuni na Mwongozo wa mwaka 2022 kwa ajili ya kusimamia biashara na kuhakikisha inakuwa rasmi kwa wadau ili iwanufaishe na kusaidia katika utunzaji wa mazingira.




# Makamu wa Rais awaasa MaRC, MaRAS kuzingatia maadili

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amewataka Wakuu wa Mikoa pamoja na Makatibu Tawala wa Mikoa kuzingatia maadili na nidhamu katika maeneo ya kazi ili kuwa picha nzuri na ya mfano kwa wengine.

Makamu wa Rais amesema hayo Agosti 22, 2023 wakati akifungua Mafunzo ya Uongozi kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa yanayofanyika katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere iliopo Kibaha Mkoani Pwani. Amesema ni lazima wakati wote wa uongozi kutafuta njia bora ya kuwashirikisha wengine ili msingi wa uongozi na utendaji uwe chachu zaidi kuleta maendeleo kwa wananchi.

Pia Makamu wa Rais amewataka viongozi wa Mikoa kuongeza jitihada kuiwezesha sekta binafsi ili iweze kukua, kushamiri na kuzalisha ajira kwa kuweka vivutio na mazingira mazuri ya uwekezaji. Amesema sekta binafsi inapaswa kuwa mshirika muhimu katika shughuli zote za maendeleo katika mikoa.

Hali kadhalika Makamu wa Rais amesema maudhui ya mada zitakazowasilishwa katika mafunzo hayo yanalenga kuondoa matukio mbalimbali yanayotokana na mapungufu katika uongozi ikiwemo kutokuzingatia mipaka ya kiutendaji kati ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wao hususan katika matumizi ya fedha pamoja na kushindwa kudhibiti uvujaji wa siri za Serikali hususan katika zama hizi za utandawazi na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Pia amewataka Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala kuzingatia masuala ya uhifadhi wa mazingira hususani kutunza vyanzo vya maji, kufuatilia fursa mbalimbali zitokanazo na shughuli za uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na biashara ya Kaboni na Uchumi wa Buluu. Amewataka kuhakikisha kunakuwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi ili kuepuka migogoro mbalimbali ndani ya jamii na kuzingatia changamoto zozote zinazojitokeza katika jamii zinashughulikiwa mapema na kwa ukamilifu.

Makamu wa Rais amesema dhima ya mafunzo hayo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020, ambayo inaelekeza umuhimu wa kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi katika hali iliyo shirikishi na yenye ubora. Ameongeza kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua umuhimu wa mafunzo hayo muhimu kwa viongozi

Kwa upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI Angellah Kairuki amesema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea viongozi hao uwezo wa kuongoza na kusimamia wananchi, fedha na rasilimali zingine muhimu za taifa. Pia amesema mafunzo hayo yatawawezesha viongozi kuwa na maamuzi ya kimkakati pamoja na kuwawezesha kuwa na uwezo katika masuala muhimu yanayohusu utekelezaji wa majukumu yao.

Ameongeza kwamba katika siku sita za mafunzo jumla ya mada 20 zinatarajiwa kuwasilishwa kwa viongozi hao ambazo zitajikita katika masuala ya uongozi, usimamizi rasilimali, miongozo na taratibu mbalimbali za utendaji kazi serikalini, usimamizi miradi na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kukuza uchumi.

# Dkt. Jafo awaasa Watanzania kuuenzi Muungano kwa kudumisha amani

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selemani Jafo ameongoza wananchi wa Mkoa wa Iringa katika kuadhimisha miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuhimiza Watanzania kuuenzi Muungano kwa kudumisha Amani.

Akizungumza na wananchi wa mkoa huo katika Uwanja wa Samora Aprili 26, 2023, Dkt. Jafo amesema kuwa matunda ya Muungano yanaonekana kutokana na muungano huo imara na wa mfano duniani ukilinganisha na nchi zingine zilizowahi kuungana na hatimaye kutengana.

Amesema kupitia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wananchi wanaishi kwa amani na mshikamano na kutokana na hali hiyo Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wa pande zote mbili za Muungano.

Waziri Jafo amesema Watanzania wanapaswa kujivunia Muungano ambao ni tunu ya taifa letu ambapo maendeleo yanapatikan kupitia miradi ya sekta mbalimbali ambayo imekuwa msaada mkubwa kwa wananchi.

"Ndugu zangu lazima tumwombee Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani tunaona miradi mingi inatekelezwa na nchi yetu inasonga mbele ambayo hakika inajenga uchumi na hayo yote ni kazi kubwa hivyo iliyofanyika chini ya uongozi wake, na tuna kila sababu ya kujivunia na kutembea kifua mbele," amesisitiza.

Katika hatua nyingine Waziri Dkt. Jafo ameupongeza Uongozi wa Mkoa wa Iringa kwa kufanya vizuri katika utunzaji wa mazingira ambao ni ajenda muhimu katika mustakabali wa nchi.

Ametoa rai kwa wananchi hususan wa Wilaya ya Mufindi kuendelea kupanda miti kwa wingi ili kunufaika na Biashara ya Kaboni ambayo tayari Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Kanuni na Mwongozo wake.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Iringa Mhe. Halima Dendego amesema katika kutekeleza maelekezo ya Serikali kuhusu kuadhimisha sherehe za Miaka 59 ya Muungano mkoa huo umeratibu shughuli za hifadhi ya mazingira.

Amesema kuwa kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wametoa jumla ya miche 89,000 lengo likiwa ni kuwakabidhi wanafunzi wa shule ili waipande na kuitunza hivyo kushiriki kikamilifu katika Kampeni ya ***'Soma na Mti'*** iliyozinduliwa na Waziri Jafo. Mhe. Dendego ameongeza kuwa bonanza hilo la michezo ni sehemu ya maadhimisho hayo ili kuwakutanisha wananchi hasa vijana na kuwajenga kiafya na uelewa kuhusu masuala ya Muungano.

Awali, Dkt. Jafo aliongoza wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Mawelewele iliyopo katika Manispaa ya Iringa, katika zoezi la kupanda miti ikiwa ni sehemu ya sherehe hizo kimkoa ambapo alipanda mti wa 11,350 kati 89,000 inayotarajiwa kupandwa mkoani humo.

Katika bonanza lililofanyika kwenye Uwanja wa Samora Waziri Jafo ambaye alikuwa mgeni rasmi alishuhudia michezo mbalimbali na kukabidhi zawadi kwa washindi ili kuleta hamasa kwa wananchi wengine kushiriki.



# Dkt. Mpango: Suala la upandaji miti ni la lazima




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akipanda mti aina ya Komamanga mara baada ya kuzindua rasmi kampeni ya kupanda miti kitaifa kwa hisani ya Benki ya NMB ikishirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) uzinduzi uliofanyika katika eneo la Mtumba Jijini Dodoma Machi 27, 2023.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema suala la kupanda miti ni lazima na kuzitaka halmashauri zote nchini kusimamia kwa karibu na kuhakikisha kwamba mazingira ya maeneo yao yanakuwa ya kijani, safi na ya kuvutia na zoezi hilo liwe endelevu.

Amesema hayo wakati wa akizindua kampeni ya kupanda miti kitaifa kwa hisani ya Benki ya NMB ikishirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), uzinduzi uliofanyika katika eneo la Mtumba jijini Dodoma Machi 27, 2023.

Mhe. Dkt. Mpango amesema wakurugenzi wa halmashauri zote nchini wanapaswa kutoa maelekezo kwa shule, taasisi mbalimbali na kwa wananchi ili washiriki kikamilifu katika uhifadhi na usafi wa mazingira.

Vilevile Makamu wa Rais ameziagiza Halmashauri kwa kushirikiana na TFS, kupanda aina za miti ambayo inaendana na mazingira ya maeneo waliopo pamoja na kuiwezesha jamii hususani ya vijana kupata elimu zaidi kuhusu utunzaji wa miti ili kuhakikisha wanachangia katika uhifadhi wa mazingira kwa weledi.

Amesema Serikali inafahamu na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na sekta binafsi pamoja na taasisi za kidini hapa nchini katika kuhakikisha utekelezaji wa mipango mbalim-

bali ya uhifadhi wa mazingira inakuwa na mafanikio.

Mhe. Dkt. Mpango ametoa wito kwa taasisi hizo kuongeza juhudi hasa katika kuhamasisha, kukuza uelewa na kujenga uwezo wa jamii na taasisi mbalimbali kuhusu hifadhi ya mazingira pamoja na kutafuta rasilimali fedha zitakazo changia utekelezaji wa Sera ya Mazingira.

Aidha, Makamu wa Rais ametoa rai kwa Benki ya NMB kuona uwezekano wa kutumia Umoja wa Mabenki (TBA) kuongeza nguvu zaidi katika kuifanya Dodoma kuwa ya kijani kwa muda mfupi zaidi kwa kutambua ndio makao makuu ya nchi.

Kwa Upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amesema ajenda ya upandaji miti nchini ni maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inayoelekeza kupanda miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri kwa lengo la jumla ya miti milioni 276.

Hali kadhalika, Mhe. Dkt. amesema kuwa kifungu cha 68 (l) kinaelekeza Mkoa wa Dodoma upandwe miti milioni 40 katika kipindi cha miaka mitano. Ameipongeza Benki ya NMB kwa jitihada wanazozifanya katika kushirikiana na Serikali kwenye uhifadhi wa mazingira.

Kamishna wa Uhifadhi TFS Prof. Dos Santos Silayo amesema Wakala utashirikiana vema na NMB kuhakikisha wanatekeleza vema adhma ya upandaji miti milioni 1 kwa kutoa miongozo mbalimbali ya kitaalamu na kushirikiana nao katika kila Nyanja kuhakikisha adhma hiyo inafanikiwa.

Aidha Prof. Silayo amesema ushirikiano baina ya NMB na TFS utasaidia katika kuongeza wigo wa upatikanaji wa miche ya miti jamii mbalimbali katika maeneo mbalimbali nchini na kuipanda kwa weledi kuhakikisha inastawi.

Ametoa wito kwa wadau mbalimbali kuendelea kujitokeza kusaidiana na serikali katika kuongeza nguvu kwenye uhifadhi katika kutekeleza kazi mbalimbali zinazopunguza utegemezi wa misitu na hasa kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa misitu, upandaji miti na kuhifadhi mazingira.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB Ruth Zaipuna amesema Benki hiyo itapanda miti milioni 1 kwa mwaka 2023 nchi nzima na kuitunza kuhakikisha inafikia lengo.

Ameongeza kwamba Benki hiyo itaendesha shindano maalum la upandaji miti mashuleni litakalofahamika kama "Kuza Mti Tukutuze" ambapo kupitia shindano hilo litakalofanyika kwa mwaka mmoja na nusu shule zitashindana kutunza miti watakayokabidhiwa na TFS.


Amesema pamoja na zawadi mbalimbali zitakazotolewa lakini pia shule itakayoweza kupanda miti 2,000 na kukuza asilimia 80 na zaidi ya miti hiyo itafanikiwa kupata zawadi ya shilingi milioni 50. Bi. Zaipuna amesema Benki ya NMB inatambua wajibu ilionayo katika jamii kuhakikisha wanatunza mazingira ili utendaji wa kazi kuwa mzuri na bora zaidi kwani mazingira yanapoharibika hakuna kundi linalobaki salama.

Katika uzinduzi wa kampeni hiyo zaidi ya miti 3000 imepandwa katika eneo la Mtumba jijini Dodoma.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo na Naibu Waziri Mhe. Khamis Hamza Khamis wakipanda mit wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kupanda miti kitaifa lililoongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Dkt. Philip Mpango.*

# MAKAMU WA RAIS ASHIRIKI KUMBUKIZI YA MIAKA 51 YA KIFO CHA SHEIKH KARUME KISIWANDUI, ZANZIBAR APRILI 7, 2023



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar kwa ajili ya kuungana na viongozi na wananchi katika kumbukizi ya Miaka 51 ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Hayati Sheikh Abeid Amani Karume iliyofanyika Afisi Kuu ya Chama Cha Mapinduzi – Kisiwandui, Zanzibar.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja viongozi mbalimbali wa Serikali, Dini na Chama katika dua ya pamoja ya kumuombea aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Sheikh Abeid Amani Karume katika kumbukizi ya miaka 51 ya kifo chake iliyofanyika Afisi Kuu ya Chama Cha Mapinduzi – Kisiwandui Zanzibar.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akiweka shada la maua katika kaburi la aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Sheikh Abeid Amani Karume katika kumbukizi ya miaka 51 ya kifo chake iliyofanyika Afisi Kuu ya Chama Cha Mapinduzi – Kisiwandui Zanzibar.*




# Makamu wa Rais ahimiza mikakati kuhifadhi rasilimali za bahari

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema zinahitajika juhudi za pamoja za ndani ya nchi za kikanda na kimataifa katika kuweka mikakati na kutafuta njia madhubuti za kulinda na kuhifadhi bahari na rasilimali zake kwa kusimamia matumizi endelevu ya bahari.

Amesema hayo wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Bahari Duniani yaliyofanyika jijini Dar es salaam Juni 8, 2023 huku akisisitiza uwiano sawia kati ya hali ya bahari na kuimarika kwa uchumi kwani Afya ya Bahari na mifumo imara ya kiikolojia ya baharini ni muhimu kwa uchumi wa buluu ambao ni sehemu ya ajenda ya nchi kufikia maendeleo endelevu.

Dkt. Mpango amesema umuhimu wa kulinda bahari na rasilimali zake unatokana na faida lukuki zinazopatikana zikiwemo bahari kuchukua zaidi ya asilimia 70 ya eneo la dunia, zaidi ya asilimia 50 ya hewa safi ya oksijeni, zaidi ya asilimia 90 ya joto la ziada linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuchukua zaidi ya asilimia 30 ya hewa ya kabonidayosaidi inayozalishwa na shughuli za kibinadamu.

Ameongeza kuwa tafiti zinaonesha kufikia mwaka 2030 Bahari itakuwa ndio nguzo kuu ya uchumi duniani ambapo takriban watu milioni 40 watakuwa wameajiriwa moja kwa moja na viwanda vinavyotumia rasilimali za bahari. Hali kadhalika amesema zaidi ya asilimia 90 ya usafirishaji wa bidhaa kimataifa hutegemea bahari pamoja na bahari ni makazi ya viumbe hai mbalimbali ambavyo ni chanzo kikuu cha protini kwa zaidi ya watu bilioni tatu duniani.

Makamu wa Rais ameongeza kwamba Tanzania ni mojawapo ya nchi chache duniani zilizojaliwa kuwa na sehemu ya bahari inayokadiriwa kuwa na ukubwa kilometa za mraba zipatazo 64,000, ufukwe wenye urefu wa kilometa 1,424 pamoja na ukanda huru wa kiuchumi (Exclusive Economic Zone) upatao kilometa za mraba 223,000 ambao unaongeza wigo wa shughuli za uchumi wa bahari. Amesema faida hiyo ya kijiografia ni adimu na adhimu kwani inaipa Tanzania nafasi kubwa ya kufaidi matunda yatokanayo na bahari pamoja na rasilimali zake.

Makamu wa Rais ameiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana Wizara ya Uvuvi na Taasisi za Utafiti wa Bahari kama Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI), Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyoko Zanzibar (IMS) kuhakikisha utafiti wa kina unafanyika kwa wingi zaidi ili kuongeza uelewa wa sayansi ya bahari pamoja na athari za changamoto zilizojitokeza kwa jamii na ikolojia.

Vilevile Makamu wa Rais amesema upo umuhimu mkubwa wa kuhusisha na kushirikishwa kikamilifu kwa jamii za asili ya pwani katika ulinzi wa rasilimali za bahari kwa kuwa wao ndio wafaidika au waathirika wa kwanza wa mazingira ya bahari. Pia ameagiza Mamlaka zinazohusika na uvuvi na uhifadhi ziongeze jitihada katika kutoa elimu zaidi kwa wavuvi ili washiriki kikamilifu katika uhifadhi wa rasilimali endelevu za bahari na kuondokana na njia zisizofaa za uvuvi.

Aidha Dkt. Mpango ametoa wito kwa vyombo vya habari na wasanii nchini kutambua wajibu walionao katika kusaidia jamii kupata uelewa wa kutosha kuhusu bahari na rasilimali zake kupitia nyenzo mbalimbali kama vile vipindi maalum, makala, mahojiano ya ana kwa ana na kurushwa kwenye redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii.


Kwa upande wake Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega amesema Wizara hiyo inatoa umuhimu mkubwa katika shughuli za uhifadhi wa rasilimali za bahari na kudhamiria kuilinda bahari na viumbe wake. Ameongeza kwamba ili kuwa na uvuvi endelevu ni lazima kuwa na maeneo ya uhifadhi baharini ambayo yanalenga katika kulinda, kuhifadhi na kudumisha uvuvi endelevu na kukuza mchango wa sekta ya uvuvi na pato la taifa.

Awali akitoa maelezo kuhusu Siku ya Bahari Duniani, Mwenyekiti wa Bodi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Nchini Mhandisi Dkt. Boniventura Baya amesema siku hiyo ya kimataifa inaunga mkono suala la utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu na kukuza maslahi ya umma katika ulinzi wa bahari na usimamizi endelevu wa rasilimali zake. Amesema vita dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa bahari inaendelea dunia nzima ikiwemo Tanzania kwa kutambua umuhimu mkubwa wa bahari kwa Maisha ya mwanadamu.

Wazo la kuanzishwa kwa Siku ya Bahari Duniani hlilipendekezwa mwaka 1992 na kutambuliwa rasmi na Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 2008. Kauli Mbiu ya Siku ya Bahari Duniani kwa mwaka 2023 ni "Sayari ya Bahari: Mawimbi Yanabadilika" (Planet Ocean: Tides Are Changing).

## BAJETI 2023/24

# Kitabu cha Muungano kuanza kutumika mashuleni




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amewasilisha bungeni Hotuba ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24.

Akiwasilisha hotuba hiyo Aprili 24, 2023, Dkt. Jafo amesema Ofisi ya Makamu wa Rais imekamilisha taratibu zote za kupata Ithibati ya Kitabu cha 'Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo' kwa ajili ya kutumika kama kitabu cha ziada kwa shule za sekondari nchini.

Amesema kitabu hicho kitasaidia kuwajengea wanafunzi uelewa kuhusu namna Muungano huu adhimu ulivyoasisiwa pamoja na faida zake ili kuulinda na kuuenzi.

Akiendelea kuwasilisha hotuba hiyo, Dkt. Jafo amesema Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya maandalizi ya kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Amefafanua kuwa lengo la kuanzisha kituo hicho ni kuwa na mfumo endelevu wa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka za Muungano ili kuongeza uelewa wa masuala ya Muungano kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Halikadhalika, Waziri Jafo amesema kuwa Ofisi itaendelea kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa pande mbili za Muungano ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Zanzibar.

Pamoja na hayo, ameongeza kuwa mafunzo ya usimamizi wa miradi inayogharamiwa na fedha za Mfuko wa Jimbo yatatolewa kwa wabunge, wakurugenzi wa halmashauri na wataalamu katika halmashauri za Zanzibar.

Aidha, Waziri Dkt. Jafo amesema kuwa Ofisi imeendelea kuhimiza umuhimu wa wizara, idara na taasisi zisizo za Muungano kuimarisha ushirikiano na kubadilishana uzoefu, sera, sheria, utaalamu na wataalamu na hadi kufikia Machi, 2023 vikao 12 vya ushirikiano vimefanyika baina ya wizara.

Pia, amesema Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu masuala ya Muungano yanayosimamiwa na wizara, taasisi na idara za Muungano kwa faida ya pande zote mbili za Muungano na



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akitoa ufafanuzi wa hoja za wabunge wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2023/24 aliyoiwasilisha bungeni jijini Dodoma Aprili 24, 2023. Kulia ni Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis.*

kuwa kati ya taasisi 33 za Muungano, 27 zina Ofisi Zanzibar na hivyo kusogeza huduma karibu na wananchi.

Dkt. Jafo amesema kutokana na hatua hiyo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na utambuzi na usajili wa wananchi katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar uliofanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na kutoa ithibati ya mitaala kwa vyuo vikuu vya Tanzania Bara na Zanzibar iliyofanywa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Ameyataja mafanikio mengine kuwa ni Udahili wa wanafunzi wa Shahada ya kwanza katika Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania Bara na Zanzibar kupitia TCU na mafunzo kwa vyuo na shule za sekondari kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa pande zote za Muungano yaliyotolewa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Kwa upande wa Hifadhi ya Mazingira Dkt. Jafo amesema katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhifadhi wa Bonde la Ruaha Mkuu, Ofisi imeshiriki katika utatuzi wa mgogoro wa ardhi katika Bonde la Mto Ruaha katika eneo la Ihefu ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Utatuzi wa mgogoro huo ulihusisha Mawaziri kutoka Wizara nane za Kisekta, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Jumuiya za Wafugaji, Wawekezaji katika mashamba ya mpunga, wakulima wadogo wa mpunga na Wananchi wa Wilaya za Mbarali na Chunya na kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango kazi huo ili kuhifadhi mazingira ya bonde hilo na ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu.

Katika kuhakikisha hifadhi endelevu ya mazingira, kwa mwaka 2023/24, Ofisi ilipanga kutekeleza vipaumbele vitano ambavyo ni kusimamia Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) na kuchukua hatua za kupunguza uharibifu wa Mazingira.

Vipaumbele vingine ni Kuimarisha usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini, Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Fursa ya Biashara ya Kaboni, Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ikijumuisha utoaji elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Sheria na Sera ya Mazingira na Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Baada ya kuwasilisha hotuba hiyo, Bunge lilijadili na kuidhinisha jumla ya Shilingi 54,102,084,000 kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Khamis Hamza Khamis wakipongezwa na mawaziri mara baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2023/24 bungeni jijini Dodoma Aprili 24, 2023.*

# RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN APOKEA TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga wakati alipowasilisha taarifa ya shughuli zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma Agosti 17, 2023.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; Chimbuko, Misingi na Maendeleo kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga, Ikulu mkoani Dodoma tarehe 17 Agosti, 2023. Kitabu hicho kimeandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.*

# RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN APOKEA TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea kitabu cha Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032) kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga, Ikulu mkoani Dodoma Agosti 17, 2023. Mpango Kabambe huo umeandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga mara baada ya kuwasilisha taarifa ya shughuli zinazofanywa na Ofisi hiyo, Ikulu mkoani Dodoma Agosti 17, 2023.*

# MATUKIO WAKATI WA UWASILISHAJI WA HOTUBA YA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS 2023/24



*Viongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wakitambulishwa wakati wa kuanza kwa kikao cha kuwasilisha Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 bungeni jijini Dodoma Aprili 24, 2023.*



*Watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais wakitambulishwa katika kikao cha kuwasilisha Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 bungeni jijini Dodoma Aprili 24, 2023.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akipongezwa na waziri mara baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 Aprili 24, 2023*



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis (katikati) akifurahia jambo na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (kushoto) pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji, na Mazingira Mhe. Jackson Kiswaga mara baada ya kupitishwa kwa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 Aprili 24, 2023.*




# Waziri Jafo asisitiza matumizi ya nishati mbadala kwa taasisi

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Seleman Jafo amezisisitiza taasisi za umma na binafsi zenye kuhudumia watu zaidi ya 100 zitumie nishati mbadala ili kupunguza kasi ya ukataji wa miti.

Ametoa msisitizo huo Aprili 19, 2023 wakati akizindua Kampeni ya Mazingira na Matumizi ya Nishati Mbadala pamoja na Mashindano ya Upandaji wa Miti katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Wasichana Ruvu wilayani kibaha mkoani Pwani.

Akizungumza wakati wa shughuli hiyo, Dkt. Jafo ametoa wito kwa wananchi kuungana katika kutunza na kulinda mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazoathiri mazingira na uchumi.

"Ndugu zangu lengo kubwa la katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi ni kusonga mbele katika kudhibiti uharibifu wa mazingira, ukataji miti na maelekezo hayo hayakugusa mwananchi mmoja mmoja licha ya kwamba wananchi wanatakiwa kutunza mazingira na kuacha kukata miti ovyo," amesisitiza.

> Ndugu zangu lengo kubwa la katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi ni kusonga mbele katika kudhibiti uharibifu wa mazingira, ukataji miti na maelekezo hayo hayakugusa mwananchi mmoja mmoja licha ya kwamba wananchi wanatakiwa kutunza mazingira na kuacha kukata miti ovyo

Aidha, Waziri Jafo amepowangeza Taifa Gas kwa kufunga mtungi wa gesi katika shule hiyo kwa ajili ya matumizi ya jiko akisema kuwa taasisi kuacha kutumia kuni na mkaa inawezekana.

Aliongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kujipambanua katika suala zima la mazingira kwa kutekeleza miradi ya kujali mazingira.

Kwa upande wake Mkuu Wilaya ya Kibaha Mhe. Nickson Simon kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani amesema Mkoa huo una changamoto kubwa ya kimazingira hivyo wameamua kujipambanua katika upande wa mazingira ili kupambana na hali hiyo.

Amesema Mkoa wa Pwani umeshapanda miti milioni tisa sawa na asilimia 82 na lengo likiwa ni kupanda miti zaidi ya milioni 13 huku akiongeza kuwa wamejipanga kuongeza usimamizi wa mazingira, upandaji miti, teknolojia mbadala na uchumi.

Bi. Angela Bhoke kutoka Taifa Gas ameeleza kuwa wanajenga kiwanda cha mitungi ya gesi katika eneo la Misugusugu lengo ni kushirikiana na Serikali katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na kuhimiza matumizi ya nishati mbadala.

# Makamu wa Rais asisitiza mkazo familia kuwa kiini cha maendeleo



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwasili katika Ukumbi wa Mikutano wa Museum of fine arts Jijini Budapest nchini Hungary kushiriki Mkutano wa Tano wa Idadi ya Watu (5th Budapest Demographic Summit) uliofanyika Septemba 14, 2023.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa mataifa kutambua umuhimu kuweka mkazo katika taasisi ya familia ya kiutamaduni ili kuifanya kuwa kiini cha maendeleo ulimwenguni.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati akihutubia kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Tano wa Idadi ya Watu (5th Budapest Demographic Summit) uliofanyika jijini Budapest nchini Hungary Septemba 14, 2023.

Amesema inahitajika nguvu ya pamoja kimataifa katika kuimarisha ustawi wa familia ikiwemo kuzingatia kanuni na desturi za kiutamaduni pamoja na kuunga mkono mafundisho ya dini ambayo yanakuza maadili ya familia na kulinda usalama na mwendelezo wa familia.

Pia, Makamu wa Rais ametoa wito kwa serikali ulimwenguni kutengeneza na kutekeleza sera, programu na sheria zitakazohakikisha usalama na uendelevu wa familia. Aidha ametoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kushirikiana na Bara la Afrika katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na ongezeko la idadi ya watu zikiwemo uhitaji wa huduma za afya na elimu, ukosefu wa ajira, upungufu wa chakula na uhamiaji haramu.

Akitoa mfano wa Tanzania katika mkutano huo wenye kauli mbiu ya "Familia Msingi wa Usalama" Makamu wa Rais amesema nchini Tanzania familia inatambuliwa kama msingi imara na muhimu ambayo ni mwanzo wa ujenzi wa mtandao wa mahusiano ya jamii nzima.

Ameongeza kwamba Tanzania familia inahusisha muunganiko wa ndoa ya watu wa jinsia mbili tofauti,watoto wao pamoja na ndugu au wategemezi wao ambapo pamoja na mambo mengine, familia hutumika kuimarisha utaratibu na utulivu katika jamii na pia husaidia katika uwezo wa kufanya maamuzi na utatuzi wa matatizo pamoja na utulivu wa kifedha, utoaji wa elimu na huduma za afya kwa wanafamilia na malezi.

Makamu wa Rais amesema pamoja na kuendelea kusisitiza na kuimarisha ustawi wa familia, serikali ya Tanzania imeendelea kuwekeza katika kujenga uchumi na kuboresha miundombinu ya kijamii kwa maendeleo ya watu ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme, elimu pamoja na utoaji wa elimu bila malipo kuanzia ngazi ya awali hadi sekondari. Ameongeza






*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akisalimiana na kuzungumza na Rais wa Hungary Mhe. Katalin Novàk wakati alipowasili katika Ukumbi wa Mikutano wa Museum of fine arts Jijini Budapest nchini Hungary kushiriki Mkutano wa Tano wa Idadi ya Watu (5th Budapest Demographic Summit) uliofanyika Septemba 14, 2023.*

kwamba serikali imeongeza jitihada katika kuwavutia vijana ambao ni idadi kubwa iliopo nchini kushiriki katika kilimo biashara kwa kuanzisha programu maalum ya Jenga Kesho iliyobora (BBT).

Halikadhalika, Makamu wa Rais amesema sababu za kiuchumi na migogoro zinazopelekea ongezeko la wahamiaji ndizo zinazopelekea athari ya mienendo ya idadi ya watu Barani Afrika. Amesema Tanzania imekuwa ikihifadhi wakimbizi zaidi ya laki nne kutoka mataifa Jirani ambao wamekua wakitafuta amani na ustawi wa Maisha yao.

*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akihutubia Mkutano wa Tano wa Idadi ya Watu (5th Budapest Demographic Summit) uliofanyika Septemba 14, 2023.*

Makamu wa Rais ametoa wito kwa kwa nchi na mataifa kuiunga mkono Tanzania katika kuwahudumia wakimbizi ambapo uwepo wao huongeza mahitaji kama vile ya ardhi, maji, huduma za kijamii na miundombinu. Pia ametoa wito wa kuboresha usalama wa kitaifa na kikanda, kuzuia migogoro, kuimarisha na kulinda amani pamoja na kuongeza juhudi katika kuzuia na kupambana na ugaidi.

Vilevile, Makamu wa Rais amesema Tanzania inathamini ushirikiano na Jamhuri ya Hungary katika nyanja ya Elimu na kuinua ujuzi. Amesema serikali imedhamiria kuimarisha uhusiano na nchi ya Hungary katika ukuzaji wa ujuzi kwa vijana, uwekezaji hususani katika kilimo na biashara ya kilimo, uongezaji wa thamani, utengenezaji wa bidhaa, utalii na teknolojia.

Mkutano huo wa siku mbili ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka mataifa mbalimbali, Watunga Sera, Viongozi wa Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, Viongozi wa Dini na Wanataaluma.




# Katibu Mkuu Maganga awataka watafiti kuweka mipango ya matumizi ya rasilimali za bahari

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga ametoa wito kwa watafiti, wataalamu na wanasayansi ya bahari kujadili kwa pamoja namna bora ya kutunza, kusimamia na kuwekeza katika rasilimali za bahari zilizopo nchini ili kuongeza mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Ametoa wito huo Machi 27, 2023 jijini Dar es Salaam wakati akifungua Warsha ya Uhakiki wa Taarifa ya Upembuzi yakinifu wa awali kuhusu Mpango wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari (MSP) kwa Nchi za Magharibi mwa Bahari ya Hindi iliyoandaliwa na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Bi. Maganga amesema kuwepo kwa mpango shirikishi wa matumizi ya maeneo ya bahari ni sehemu ya suluhisho la kuleta matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na kufungua fursa za kiuchumi na ajira kwa kuzingatia utunzaji sahihi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Kuna fursa nyingi katika matumizi ya bahari ambazo zikifanyika kwa namna endelevu zitachangia katika ukuaji wa uchumi. Shughuli kama vile uvuvi mdogo, uvuvi wa bahari kuu, ufugaji samaki na mazao ya baharini zina mchango mkubwa katika kukuza Uchumi wa Buluu na hatimaye kukuza uchumi wa nchi," amesema Bi. Maganga.

Aidha, ameeleza kuwa Malengo ya Umoja wa Mataifa hasa lengo Namba 14 la Maendeleo Endelevu linasisitiza matumizi endelevu ya bahari, ambapo lengo hilo linakwenda sambamba na malengo ya warsha hiyo inayohimiza kupitia na kuhakiki taarifa ya upembuzi yakinifu wa awali wa Mpango wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari.

Akifafanua zaidi Maganga amesema kuwa Mpango huo umekuja katika wakati mwafaka ambapo Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar zikiwa zimejipanga katika kupanua wigo wa matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake ili ujenga uchumi imara.

Ameongeza kuwa mafanikio ya Uchumi wa Buluu yanategemea uwepo kwa Mpango Mahsusi wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari, hivyo Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)kwa kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar zitaendelea kushirikiana na wadau katika kuratibu na kushiriki katika utekelezaji wa Mpango huo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la The Nature Conservancy kutoka Ujeruamani Bi. Lucy Maghembe amesema washa hiyo imewakutanisha wadau mbalimbali wa masuala ya sayansi ya bahari waliokutana kwa ajili ya kujadili sera na mipango endelevu ya usimamizi wa rasilimali za bahari na namna bora ya kushughulikia migongano ya matumizi ya rasilimali za bahari.

"Katika Afrika Tanzania tunakuwa taifa la nne kuwa na Mpango wa aina hii. Mataifa mengine ya Kenya, Shelisheli na Mauritius zimeanza utekezaji wa Mpango huu. Tumejipanga kuja na sera na mipango imara itakayosaidia usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari katika ukanda wa bahari ya Hindi.

Naye Mtaalamu wa Sayansi ya Bahari, Profesa Yunus Mgaya amesema wa wanasayansi umebaini kuongezeka kasi ya matumizi ya rasilimali za bahari katika Ukanda wa Bahari ya Hindi hatua inayochangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa shughuli za kijamii na kiuchumi ikiwemo nishati, gesi, utalii n.k

"Utafiti uliofanyika umetoa mapendekezo ya kuwa na mifumo ya kitaasisi inayosaidia usimamizi na uhifadhi endelevu wa rasilimali za bahari ili kuweza kuzuia migogoro na migongano baina ya watumiaji wa rasilimali zilizopo baharini" amesema Prof. Mgaya.

Mkurugenzi Idara ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Zahor Alharousy amesema kupitia Mpango huo uliobuniwa na wataalamu utaiwezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupanua wigo na fursa za ukuaji wa uchumi kwa wananchi hususani wavuvi na wakulima wa zao la mwani.

Tumejipanga kikamilifu kuhakikisha Mpango unaondaliwa unakuja na mipango endelevu ya matumizi ya rasilimali za bahari na kuibua fursa kwa wakulima na wavuvi"

Warsha hiyo imeandaliwa na Shirika la The Nature Conservancy (TNC) kutoka Nchini Ujeremani inashirikisha wadau, wafadhili na mashirika ya kimataifa yanaohusika katika usimamizi, matumizi na uwekezaji katika fukwe za bahari, maziwa na mito.



# Dkt. Jafo: Fanyeni tafiti zitakazotoa ufumbuzi wa mabadiliko ya tabianchi

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo ametoa rai kwa watafiti kufanya tafiti zitakazosaidia kupata ufumbuzi wa changamoto za kimazingira hususan mabadiliko ya tabianchi.

Ametoa rai hiyo wakati akizindua Programu ya Utafiti kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) Oktoba 11, 2023 jijini Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo Tanzania imenufaika na zaidi ya shilingi bilioni 9 zilizotolewa na Serikali ya Norway kupitia Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD) katika makubaliano yaliyosainiwa na Serikali hizo mbili kwa ajili ya kufanya utafiti huo.

Waziri Jafo amesema kuwa uchumi unaweza ukaathirika kutokana na changamoto za kimazingira ambapo jamii hushindwa kufanya shughuli za kujipatia kipato ikiwemo kilimo na ufugaji kutokana na ukame

Amesema katika kukabiliana na changamoto hiyo watafiti wanatarajiwa kutoa majawabu kuhusu sekta gani itasaidia katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Maeneo haya tuna kazi kubwa ya kujua ni tafiti zipi kwa mfano kama ni kilimo gani kinaweza kufanyika katika maeneo yanayokabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, ninyi watafiti mna jukumu kubwa la kutusaidia katika hili," amesema.

Ameishukuru Serikali ya Norway kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na kusema kuwa hayo ni matunda ya diplomasia ya Mwanamazingira namba moja Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Niwapongeze COSTECH na Serikali ya Norway kwa kushirikiana na Tanzania kwa upande wa research (utafiti) kwasababu tuna changamoto kubwa za athari za mabadiliko ya tabianchi na ndio maana tulijiwekea malengo ya kupunguza emission ifikapo kwa asilimia 30 hadi 35," amesema.



# Mitawi: Vyombo vya Habari ni Wadau muhimu wa Elimu ya Mazingira

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imesema itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari nchini katika kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira ikiwemo wa uhifadhi wa Tabaka la Ozoni.

Hayo yamesemwa na Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Mitawi wakati akifungua warsha ya mafunzo kwa waandishi wa vyombo vya habari kuhusu udhibiti wa uingizaji wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal iliyofanyika Septemba 16, 2023 jijini Dar es Salaam.

Mitawi amesema Tanzania kama nchi nyingine Duniani imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na athari za matumizi ya vifaa vya kemikali vyenye ukomo wa matumizi kwa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa kemikali hizo zinazodhibitiwa ambazo zina madhara mbalimbali katika jamii ikiwemo magonjwa, ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi.

"Tutaendelea kushirikiana na vyombo vya habari katika kuhakikisha elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira inaifikia jamii...Tunatambua mchango mkubwa wa JET (Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira) kwani tangu kuanzishwa kwake mwaka 1991 imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha jamii kutunza na kuhifadhi mazingira" amesema Mitawi.

Akifafanua zaidi Mitawi amesema ni takribani miaka 35 sasa tangu Jumuiya ya Kimataifa ipoamua kuchukua hatua mahsusi za kunusuru tabaka la ozoni katika kulinda afya ya binadamu na mazingira ambapo mwaka 1987 ilipitishwa Itifaki ya Montreal kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka hilo.

"Lengo kuu la Itifaki hii ni kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni....Nafasi ya vyombo vya habari ni kubwa katika kuelimisha jamii kuhusu athari ya matumizi ya kemikali hizi ambapo zimeleta athari mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi" amesema Mitawi.

Amesema katika jitihada za kuhifadhi tabaka la ozoni, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa na kutekeleza programu na shughuli mbalimbali ikiwemo kuendelea kuhimiza jamii kupunguza shughuli za kibinadamu ambazo zinasababisha mabadiliko ya tabianchi pamoja na kutoa mafunzo kwa Maafisa Forodha na Wasimamizi wa Sheria maeneo ya mipakani.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Kemilembe Mutasa amesema juhudi mbalimbali zimeendelea kufanywa na Serikali katika kulinda Tabaka la Ozoni.

"Tanzania sio mzalishaji wa kemikali hizi...Tumekuwa tukipokea kutoka nchi za nje..Tumeandaa kanuni, sera, sheria na miongozo mbalimbali katika kuelimisha jamii na pia Tumekuwa na mfululizo wa mafunzo haya kwa makundi mbalimbali ili kudhibiti kemikali hizi" amesema Kemilembe.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Bi. Mariam Mziwanda ameishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuandaa mafunzo hayo na kutambua mchango wa vyombo vya habari katika kutoa elimu kuhusu udhibiti wa tabaka la ozoni katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Suala la usimamizi wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira halipaswi kuachiwa Serikali pekee ...Ni wajibu wetu sote kuunga mkono juhudi hizo... tunaishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kutambua nafasi ya vyombo vya habari katika kufikisha elimu ya uhifadhi wa tabaka la ozoni kwa jamii" amesema Mariam.

Tarehe 16 Septemba kila mwaka, Tanzania huungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni . Kauli mbiu ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni mwaka 2023 ni ***"Hifadhi ya tabaka la ozoni na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi."***



*Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi (kulia) akibadilishana mawazo na washiriki wa mafunzo kuhusu udhibiti wa uingizaji wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal akiwemo Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Bi. Jocye Shebe (kushoto) na Mwandishi wa Habari wa Kampuni ya Uhuru Media Group Bi. Mariam Mziwanda mudi mfupi baada ya kufungua warsha hiyo.*




# Waziri Jafo: Wananchi tunzeni miradi na kulinda mazingira

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amewataka wananchi kulinda miradi ya maendeleo, hifadhi ya mazingira kwa kupanda miti pamoja na kulinda uoto wa asili ili iendelee kudumu.

Ametoa rai hiyo Mei 3, 2023 wakati akizindua miradi mbalimbali kupitia Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR) unaoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

Dkt. Jafo amezindua miradi hiyo yenye thamani ya shilingi milioni 520 ikiwemo uchimbaji wa visima viwili virefu vya maji inayojumuisha mfumo wa sola kwa ajili ya kuvuta maji, matanki ya kuhifadhi maji pamoja na mfumo wa umwagiliaji na wa matumizi ya wananchi.

Miradi mingine ni lambo la lenye uwezo wa kukusanya maji lita za ujazo 252,299 zikiweza kumwagilia hekta 287 za mazao ya mbogamboga, kiwanda kidogo cha sabuni na kikundi cha uzalishaji uyoga.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na wananchi wa vijiji vilivyonufaika na mradi vya Melela, Magali na Mingo, amesema kuwa Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha wananchi katika maeneo yenye ukame wanapata mafanikio.

Amesema kuwa Serikali inapeleka miradi kwa wananchi ili kuwasaidia katika kupata fursa za kimaendeleo pamoja licha ya kuwepo kwa changamoto za mabadiliko ya tabiachi zinazochangia ukame.

"Ndugu zangu niwashukuru sana kwa kutekeleza hii miradi na niwaombe tuilinde asitokee mharibifu akaja kuharibu miundombinu tumsimfumbie macho, lakini pia ajenda yetu kuu tutunze mazingira, usipoyatunza na kuyashughulikia mazingira yatakushughulikia", amesisitiza.

Kutokana na hali hiyo hivyo, Dkt. Jafo amewapongeza viongozi katika wilaya hiyo kwa usimamizi mzuri wa miradi na kuwa wananchi wanaponufaika nayo ni jambo jambo la heri.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mvomero Mhe. Judith Nguli amemshukuru Waziri Jafo kwa kutembelea wilaya hiyo na kuzindua miradi hiyo kwa manufaa ya wananchi.

Mhe. Judith ameahidi kwa kushirikiana na timu yake kuisimamia na kuilinda miradi hiyo ya maendeleo kwa nguvu zote kuhakikisha inakwenda kwa wananchi kama ambavyo Serikali inaagiza.

Amesema kuwa wilaya yake inatekeleza shughuli za hifadhi ya mazingira ili kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa kuhakikisha inatoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda mazingira.

Baadhi ya wananchi wakiwemo Bw. Fortunata Mathias, Said Salum na Mohamed Seif Diwani wa Kata ya wameishukuru Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutekeleza Mradi wa EBARR katika eneo hilo.

Wamesema kuwa kupitia mradi wa vitalu nyumba vilivyozinduliwa wataweza kujihusisha na kilimo cha mbogamboga hivyo kujipatia kipato tofauti na hao awali amapo walishindwa kufanya shughuli za kilimo wakati wa kiangazi.

"Sisi wakulima tuliteseka sana kutokana na shida ya maji iliyosababishwa na ukame lakini sasa hivi tunafanya kazi vizuri tunamwagilia mazao yetu, tunaomba Serikali iongeze mabwawa ili tuweza kulima zaidi," amesema.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza wakati wa zoezi la upandaji miti kando ya barabara jijini Dodoma Januari 10, 2023.*

# Dkt. Jafo: Wakuu wa Mikoa, Wilaya simamieni zoezi la upandaji miti

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amewataka wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia zoezi la upandaji miti katika maeneo yao ili kufikia lengo lililowekwa na Serikali.

Pia, amewataka viongozi wa majiji na manispaa kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuwa na miti ya kutosha kando ya barabara zinazopopita katika maeneo yao ili kuhifadhi mazingira.

Dkt. Jafo ametoa kauli hiyo Januari 10, 2023 wakati akiongoza zoezi la upandaji miti kando ya barabara jijini Dodoma ikiwa ni Wiki ya Maadhimisho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Amesema baada ya nchi yetu kukumbwa na ukame katika baadhi ya maeneo ni vyema sasa wananchi wakatumia mvua hizi zinazoendelea kunyesha kupanda miti ya kutosha katika maeneo yetu na kwenye vyanzo vya maji.

"Viongozi twendeni tukasimamie wilaya zetu kupanda miti milioni moja na laki tano kwa kila halmashauri ili tufikie lengo la kupanda miti milioni 276, jambo hili tutalifanikisha kwa kutumia mvua hizi za kupandia, hapa nataka niwapongeze Dodoma mmeonesha mfano na ndani ya miaka mitatu mtakuwa jiji la mfano kwa utunzaji mazingira," amesema.

> **Viongozi twendeni tukasimamie wilaya zetu kupanda miti milioni moja na laki tano kwa kila halmashauri ili tufikie lengo la kupanda miti milioni 276,**

Akiendelea kuzungumza na wananchi pia Waziri Jafo amewataka wataalamu wa kilimo wabainishe aina za miti ipandwe katika maeneo gani ili kueupuka changamoto ya baadhi ya miti kufa.

Aidha, amewataka wakuu wa shule nchini kuhakikisha kila mwanafunzi anayeandikishwa shuleni kuhakikisha anapewa mti mmoja wa kupanda ili kuendana na Kampeni ya 'Soma na Mti' ambayo inalenga kupanda miti zaidi ya milioni 14.5.

Sanjari na hilo pia amesisitiza kila mwananchi anayeomba kibali cha ujenzi wa nyumba hakikishe anakuwa na mpango wa kupanda miti angalau mitatu na kuendelea ili tuwe na miti ya kutosha hivyo azma ya kupambana na athari z mabadiliko ya tabianchi inafanikiwa.

Zoezi la upandaji miti limehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri, wanafunzi, wadau wa mazingira na wananchi kwa ujumla.



# Serikali: Hakuna changamoto mpya za Muungano

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis amesema kuwa hadi sasa hakuna changamoto mpya za Muungano zilizojitokeza.

Amesema hayo Mei 17, 2023 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum Mhe. Angelina Adam Malembeka aliyetaka kufahamu changamoto gani mpya za Muungano zimejitokeza.

Mhe. Khamis amesema kuwa Muungano umeendelea kuimarika ambapo wananchi wa pande zote mbili wameendelea kunufaika kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Akiendelea kujibu swali hilo amesema mafanikio ya kutokuwa na changamoto mpya ni kutokana na jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuweka Mwongozo mzuri wa kushughulikia changamoto kwa haraka zinapojitokeza katika hatua za awali.

"Lengo la Serikali zote mbili ni kuhakikisha changamoto za Muungano zinazojitokeza zinapatiwa ufumbuzi na kuendelea kuimarisha Muungano ili kuepusha changamoto mpya kujitokeza," amesisitiza Naibu Waziri Khamis.

> **Lengo la Serikali zote mbili ni kuhakikisha changamoto za Muungano zinazojitokeza zinapatiwa ufumbuzi na kuendelea kuimarisha Muungano ili kuepusha changamoto mpya kujitokeza... Fedha za Mfuko wa Jimbo hutolewa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Sura 96 ya mwaka 2009 na zinatumika kwa kuzingatia Miongozo, Kanuni na Taratibu za usimamizi wa fedha za umma.**

Akijibu swali la Mbunge wa Mwera Mhe. Zahor Mohamed Haji aliyeuliza kwanini Halmashauri ya Magharibi 'A' imeweka Sheria ya Kodi na VAT kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Mhe. Khamis amesema SJMT itashirikiana na SMZ kufuatilia utaratibu unaotumika.

Amesema Fedha za Mfuko wa Jimbo hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Sura 96 ya mwaka 2009 na zinatumika kwa kuzingatia Miongozo, Kanuni na Taratibu za usimamizi wa fedha za umma.

Hata hivyo, Naibu Waziri Khamis amebainisha kuwa kila upande wa Serikali zote mbili una utaratibu wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma huku akisisitiza kuwa dhamira ya Serikali ni kuendelea kutoa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa pande zote mbili kwa ajili ya kuboresha huduma za jamii na kuwaletea wananchi maendeleo.



# Tanzania, Japan zajadili ushirikiano hifadhi ya mazingira



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Japan nchini Tanzania Mhe. Yasushi Misawa Ikulu Chamwino mkoani Dodoma Oktoba 18, 2023.

Katika mazungumzo hayo, viongozi hao wamejadili kuhusu ushirikiano wa nchi hizo mbili katika uhifadhi wa mazingira, utaalamu katika Biashara ya Kaboni pamoja na teknolojia bora katika sekta ya Uchumi wa Buluu.

Makamu wa Rais ameishukuru Serikali ya Japan kwa ushirikiano imara uliopo tangu Uhuru mwaka 1961 na kusema Tanzania inatambua mchango wan chi hiyo katika kuunga mkono juhudi za maendeleo hususani katika ujenzi wa miundombinu, maji, sekta ya elimu pamoja na masuala mbalimbali ya ushirikiano.

Aidha, Mhe. Dkt. Mpango mesema kupitia Mkutano wa Kimataifa wa Maendeleo ya Japan na Afrika (TICAD) Tanzania imenufaika kupitia programu mbalimbali na dhamira ya serikali ni kuendelea kushirikiana kwa karibu na serikali ya Japan kwa manufaa ya pande zote mbili.

Makamu wa Rais amesisitiza kuimarishwa ushirikiano zaidi wa Tanzania na Japan katika biashara, uwekezaji, utalii, matibabu ya kibingwa, mafunzo katika utalaamu na ubobezi wa masuala ya afya pamoja na vifaa tiba na dawa.

Kwa upande wake Balozi wa Japan Mhe. Misawa amesema katika kuendelea kuimarisha ushirikiano uliyopo baina ya mataifa haya mawili, tayari yameanzishwa majadiliano ya kibiashara baina ya Tanzania na Japan (Bilateral Bussiness Dialogue) kwa lengo la kuimarisha biashara kwa pande zote mbili.

Ameongeza kwamba Japan imeendelea kushirikiana na Tanzania katika sekta ya afya ikiwemo Shirika binafsi la TOKUSHUKAI MEDICAL GROUP ambalo limekuwa likishirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma na pia limeijengea uwezo Hospitali ya Benjamin Mkapa kufanya huduma ya upandikizaji figo.

Pia amesema ipo dhamira ya ujenzi wa kituo cha matibabu ya figo kitakachosaidia mikoa mbalimbali pamoja na nchi za jirani pamoja na uwekezaji katika matibabu ya kibingwa ya upasuaji ubongo (Neurosurgery).

Aidha Balozi Misawa amesema Japan itaendelea kuwa mdau wa utalii nchini Tanzania ambapo idadi kubwa ya raia wa nchi hiyo wanadhamiria kutembelea na kupanda mlima Kilimanjaro.

# Naibu Waziri Khamis ahamasisha vijana kuchangamkia biashara ya Kaboni






Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis ametoa wito kwa vijana nchini kuchangamkia fursa zinazopatikana katika Biashara ya Kaboni.

Ametoa rai hiyo wakati wa mdahalo uliohusu 'Nafasi ya vijana katika Utunzaji wa Mazingira' ikiwa ni sehemu ya Wiki ya Vijana Kitaifa, Oktoba 13, 2023 mjini Babati mkoani Manyara.

Mhe. Khamis amesema biashara hiyo inaingiza fedha nyingi hivyo vijana wanapaswa kupewa elimu ya namna inavyofanyika, hatua itakayosaidia kuwapa uelewa wa kushiriki kikamilifu.

"Biashara hiyo unaweza usiielewe usipopata elimu husika na ni biashara inayoingiza fedha nyingi za kigeni, napenda kuwaambia kwamba Serikali ipo tayari kuwaelimisha na kuwahamasisha vijana," amesema.

Aidha, Naibu Waziri Khamis amesema elimu ya kisayansi kuhusu Biashara ya Kaboni inatolewa katika Kituo cha Kitaifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni (NCMC) kilichopo mjini Morogoro.

Pia, amewakumbusha vijana kuendelea kulinda amani akieleza kuwa mataifa mengi amani inaharibika huku chanzo kikubwa kwa namna amoja au nyingine kikiwa ni vijana hivyo.

"Amani ya Nchi yetu ya Tanzania ipo kwa wananchi lakini kubwa ni vijana, jambo la kuenzi kiongozi, kuhakikisha afya njema halitokuwa kama hakutakuwa na amani ya kutosha, hivyo tusipoituza nchi yetu hawezi kutoka mtu nje akaja kuitunza na kuendeleza amani yetu."

# Makamu wa Rais awataka viongozi sekta za mazingira kukaza buti kukabili mabadiliko ya tabianchi



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amezitaka sekta zinazohusika na uhifadhi wa mazingira kujipanga upya na kuweka mikakati ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira Oktoba 19, 2023 jijini Dodoma.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati wa kikao kazi na viongozi mbalimbali wa serikali wanaohusika na sekta ya mazingira nchini, kikao kilichofanyika mkoani Dodoma. Amesema ni lazima kuweka utaratibu wa wadau wa mazingira pamoja na sekta zote muhimu husika kukutana mara kwa mara kwa lengo la ufuatiliaji wa maagizo na mipango uliyowekwa katika uhifadhi wa mazingira.

Makamu wa Rais ameagiza wakuu





wa Mikoa nchini kuongeza jitihada za kuhakikisha usafi katika maeneo yao unafanyika kikamilifu. Amesema ni vema utaratibu wa kutumia siku za mwisho wa juma katika kufanya usafi wa pamoja kurudishwa ikiwemo katika maeneo ya barabara kuu ambayo yanakabiliwa na uchafuzi wa taka za plastiki kwa wingi.

Aidha ameagiza kuwekwa kwa utaratibu maalum wa ufuatiliaji wa uhifadhi wa taka katika usafiri wa umma ili kudhibiti uchafuzi unaofanywa na watoa huduma hiyo ya usafiri katika maeneo mbalimbali.

Halikadhalika Makamu wa Rais ameagiza Wakuu wa Mikoa kusimamia zoezi la kusafisha mitaro ikiwa ni njia ya kuimarisha usafi wa mazingira pamoja na kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua za el nino zilizotabiriwa.

Pia Makamu wa Rais ameagiza kampeni za upandaji miti na usafi wa mazingira kuwa endelevu na kuhakikisha ufuatiliaji unafanyika wakati wote ili miti inayopandwa iweze kufikia lengo lililokusudiwa. Ameagiza zoezi la utoaji tuzo na motisha kwa wale wanaohifadhi vema mazingira kufanyika kikamilifu.

Makamu wa Rais ameagiza Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kuharakisha uzalishaji wa miche ya kutosha pamoja na kuwa mstari wa mbele kutoa ushauri wa aina ya miche inayopaswa kupandwa kulingana na maeneo husika.

Makamu wa Rais amesisitiza elimu kwa wananchi kuendelea kutolewa kuhusu uhifadhi wa mazingira pamoja na kudhibiti uandaaji mashamba kwa kuchoma moto bila tahadhari hali inayopelekea athari kubwa kwa binadamu,viumbe hai na mazingira.

Kikao hicho kimehudhuriwa na viongozi kutoka Wizara mbalimbali, wataalamu kutoka idara mbalimbali za serikali, Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Viongozi wa Mkoa wa Dodoma pamoja na viongozi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami - Ruvu.






*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akizungumza wakati wa Mkutano wa Uzinduzi wa Kampeni ya Jopo la Viongozi wa Juu kuhusu Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji Barani Afrika uliyofanyika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa New York nchini Marekani. Mkutano huo umeongozwa na Mwenyekiti Mwenza wa jopo la viongozi wa juu wa programu ya uwekezaji katika sekta ya maji barani Afrika ambaye ni Rais wa Senegal Macky Sall pamoja na Mwenyekiti Mwenza mbadala wa jopo hilo, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.*

# Dkt. Mpango ahimiza ushirikiano uwekezaji sekta ya maji

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema ushirikiano unahitajika baina ya serikali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo, taasisi za fedha za ndani, azaki pamoja na taasisi za elimu na utafiti ili kuitekeleza vema kampeni ya uwekezaji katika sekta ya maji barani Afrika.

Amesema hayo alipomwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Uzinduzi wa Kampeni ya Jopo la Viongozi wa Juu kuhusu Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji Barani Afrika uliofanyika kando ya Mkutano wa Baraza Kuu la 78 la Umoja wa Mataifa Jijini New York nchini Marekani Septemba 20, 2023.

Mhe. Dkt. Mpango ametoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kushirikiana na Tanzania katika kukusanya rasilimali fedha ili kukamilisha uwekezaji katika sekta ya maji kwa kuzingatia tayari Tanzania imedhamiria kukusanya takribani asilimia 43 ya rasilimali fedha kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ili kufanikisha uwekezaji huo.



Amesema Tanzania kama moja ya watekelezaji wa programu hiyo imeandaa programu ya uwekezaji katika sekta ya maji (TanWIP) ambayo inatarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka 2024 - 2030. Ametaja malengo ya uwekezaji huo ni pamoja na kuhakikisha usalama wa maji wa Taifa, uhimilivu katika athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na upatikanaji wa maji ya kutosha.

Makamu wa Rais amesema kampeni ya uwekezaji katika sekta ya maji ilioyozinduliwa Jijini New York itasaidia kukusanya rasilimali zinazohitajika zaidi kwaajili ya utekelezaji wa programu ya uwekezaji katika sekta ya maji Barani Afrika. Amesema uwekezaji katika sekta ya maji utahitaji kuongezwa ili kufikia sehemu ya malengo ya maendeleo endelevu inayohusiana na maji safi na salama.

Mkutano huo umeongozwa na Mwenyekiti Mwenza wa jopo la viongozi wa juu wa programu ya uwekezaji katika sekta ya maji barani Afrika Rais wa Senegal Macky Sally pamoja na Mwenyekiti Mwenza mbadala wa jopo hilo Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Kampeni hiyo imezinduliwa kwa lengo la kukusanya dola za marekani bilioni 30 ikiwa na kauli mbiu isemayo "Mind the gap – Invest in Water"



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (wa pili kulia) akishiriki Mkutano Mkuu wa Saba wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) uliofanyika Vancouver nchini Canada kuanzia Agosti 22 hadi 26, 2023. Kulia ni aliyekuwa Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Thomas Bwana.*

# Tanzania yasisitiza Mikakati Hifadhi ya Bionuai Mkutano wa GEF



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (wa pili kushoto) akizungumza na Naibu Mtendaji Mkuu wa shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) Bi. Elizabeth Mrema (kulia) aliposhiriki Mkutano Mkuu wa Saba wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) Vancouver Canada Agosti 22 hadi 26, 2023. Kushoto ni aliyekuwa Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Thomas Bwana.*

Tanzania imepokea na kupongeza azimio la kuanzishwa kwa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) na kusisitiza kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Dunia wa Kuhifadhi Bioanuai kupitia Mikakati ya Kitaifa ya Kuhifadhi Bionuai.

Hayo yamebainishwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga wakati wa Mkutano Mkuu wa Saba wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) unaofanyika Vancouver nchini Canada.

Pamoja na kuzipongeza nchi zilizotoa ahadi ya kuchangia Mfuko huo, Tanzania imeziomba nchi zilizoendelea na zinazoendelea kuwezesha ukusanyaji wa fedha za kutosha katika Mfuko husika.

Mfuko wa Mazingira wa Dunia ni moja ya Mifuko wa Kimataifa inayowezesha shughuli mbalimbali za uhifadhi wa mazingira duniani hususan katika nchi zinazoendelea.

Shughuli zinazowezeshwa ni pamoja na Hifadhi ya Bioanuai, Mabadiliko ya Tabianchi, Matumizi bora ya Ardhi, Udhibiti wa Taka hatarishi na Kemikali pamoja na Hifadhi ya maji yanayovuka mipaka. Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazofaidika na mfuko huu katika kuwezesha shughuli za kuhifadhi mazingira nchini.

Pamoja na mambo mengine, moja ya masuala muhimu yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa GEF ni kuanzishwa kwa Mfuko wa Dunia wa Kuhifadhi Bioanuai.

Watalaamu wengine kutoka Tanzania walioshiriki ni Mshauri wa Rais Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira Dkt. Richard Muyungi, aliyekuwa Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Thomas Bwana, Afisa Mazingira Mwandamizi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Bw. Thomas Chali na Bw. Charles Faini wa Ubalozi wa Tanzania nchini Canada.

Mkutano huo ulifunguliwa tarehe Agosti 22, 2023 na kuhitimishwa Agosti 26, 2023.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akizungumza katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es salaam ulikofanyika Mkutano wa Kimataifa wa Zao la Korosho, Oktoba 11, 2023

# Dkt. Mpango: Timizeni lengo la kutouza korosho nchi za nje

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa Wizara ya Kilimo hapa nchini kufanikisha lengo lililowekwa na Wizara hiyo la kuacha kuuza Korosho ghafi nje ya nchi ifikapo mwaka 2026.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Zao la Korosho uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar es salaam. Amesema kuendelea kuuza korosho isiyochakatwa (ghafi) kunasababisha kupunguza ajira za watanzania, kupunguza mapato ya fedha za kigeni pamoja na upatikanaji wa bidhaa zitokanazo na zao la korosho kama vile maziwa, mvinyo, juisi na mafuta.

Aidha Makamu wa Rais amesema ni muhimu mkutano huo ukajadili na kubadilishana uzoefu wa namna ya kuimarisha huduma za ugani na utoaji pembejeo kwa wakati ili kuongeza uzalishaji wa zao la Korosho.

Pia Makamu wa Rais ametoa wito kwa mkutano huo kujadili namna bora ya kuwa na mkakati wa kufikia masoko ya zao la korosho kwa usawa. Amesema kumekuwa na ulaghai kati ya wanunuzi,wasafirishaji na madalali jambo linalothibitishwa na idadi ndogo ya wanunuzi kwenye minada ambao wana ufahamu wa kutosha kuhusu bei za soko huku wakulima wa korosho wakiwa na taarifa ndogo za soko. Ameongeza kwamba kutokana na hali hiyo, wakulima wa zao la korosho wamekabiliwa na bei isiyo ya haki.


Makamu wa Rais amewakaribisha wawekezaji kuwekeza katika sekta ya zao la korosho kutokana na taifa kuwa na ardhi ya kutosha ya kilimo na hali nzuri ya hewa. Ameongeza kwamba kipindi cha mavuno ya korosho nchini Tanzania (Septemba-Desemba) ni msimu wa kutokuwepo kwa wazalishaji wengine wakuu kama vile India, Vietnam na Afrika Magharibi hivyo kutoa fursa kubwa ya soko la zao hilo.

Halikadhalika Makamu wa Rais ametoa wito kwa nchi za Afrika kujitahidi kupunguza bei ya mlaji wa korosho ili kukuza ongezeko la matumizi ya korosho na bidhaa zitokanazo na zao hilo kitaifa na kikanda. Amesema kwa kuzingatia uwezo mkubwa wa soko wa Afrika wa takriban watu bilioni 1.4 chini ya ukanda huru wa biashara barani Afrika (AfCFTA). Aidha amezisihi nchi zinazolima korosho barani Afrika kuangalia na kukomesha vitendo viovu katika biashara hiyo kama vile upangaji usio sawa wa madaraja ya korosho na usambazaji wa viuatilifu visivyofaa.

Mkutano huo wa siku tatu (Tarehe 11-13 Oktoba 2023) unashirikisha Zaidi ya wadau 500 kutoka nchi 33 zinazozalisha na kula korosho. Pamoja na mambo mengine lengo la Mkutano huo ni kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akizungumza na wauzaji wa zao la korosho kuhusu umuhimu wa kuzingatia soko la ndani ya nchi na Afrika wakati akitembelea mabanda ya maonesho yaliyopo katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar es salaam ulikofanyika Mkutano wa Kimataifa wa Zao la Korosho, Oktoba 11, 2023)




# 'Serikali iko tayari kuwashirikisha wafanyabishara ndani, nje'



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema serikali ya Tanzania ina dhamira ya dhati ya kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na jumuiya ya wafanyabiashara wa ndani ya nchi na wale wa kimataifa ili kukuza uwekezaji wa sekta binafsi.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati alipofanya mazungumzo na Taasisi ya Kimkakati kwa Biashara za Kimataifa na Serikali ya nchini Marekani (BCIU), jijini New York Septemba 23, 2023.

Amesema nchini Tanzania sekta binafsi ni mshirika mkuu wa maendeleo na taifa lipo tayari kwaajili ya biashara hivyo amewakaribisha wafanyabishara hao kuwekeza Tanzania na kutumia fursa zilizopo ili kuiwezesha nchi kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Makamu wa Rais amesema Tanzania ni nchi yenye mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji kusini mwa jangwa la sahara ikiwa na kasi ya ukuaji kiuchumi, amani, miundombinu ya nishati kutoka katika vyanzo mbalimbali, ardhi ya kutosha ya kilimo na hali ya hewa rafiki, kuimarishwa kwa mtandao wa usafiri na usafirishaji ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa pamoja na huduma nyingi zinazovutia uwekezaji na biashara.

Amesema Tanzania inawakaribisha wawekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya afya kama vile ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa vifaa tiba na dawa kwa kuzingatia uwepo wa soko katika ukanda nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kuwekeza katika kilimo, nishati,sekta ya usafiri na usafirishaji pamoja na miundombinu ya tehama.

Pia, amewakaribisha kutumia vyema ukuaji wa sekta ya viwanda vya ngozi ikizingatiwa Tanzania ni nchi ya pili kwa idadi kubwa ya mifugo barani Afrika. Pia amesema Tanzania ni nchi ya nne barani Afrika kwa uzalishaji mkubwa wa pamba (baada ya Mali, Burkina Faso, na Misri) na nchi ya nne kwa uzalishaji wa pamba asilia Duniani (baada ya India, China, na Uturuki).

Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Mpango amesema kwa sasa uwezo wa usindikaji wa pamba umeongezeka na kwa sasa zinasafirishwa nguo hadi nchini Marekani chini ya mpango wa AGOA.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi na Mwanzilishi wa Taasisi ya Doris Mollel kuhusu vifaa tiba kwaajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (Njiti) vilivyotolewa na taasisi hiyo katika Hospitali ya Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma. Tarehe 06 Julai 2023.*

# Wenzi wenu wawasindikize kliniki – Dkt. Mpango

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa wajawazito kusindikizwa na wenzi wao kuhakikisha wanahudhuria kliniki wakati wote wa ujauzito ili kuweza kutambua mapema magonjwa na kuepukana na hatari za kuzaliwa mtoto kabla ya wakati.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati wa hafla ya makabidhiano ya vifaa tiba kwa ajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti) vilivyotolewa na Taasisi ya Doris Mollel pamoja na vifaa tiba vilivyotolewa na Tume ya Ushindani (FCC) katika Hospitali ya Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma Julai 20, 2023.

Amekemea tabia za ukatili hususani kuwapiga wanawake wajawazito kwani madhara yake ni makubwa katika kupatikana kwa mtoto. Ametoa rai kwa viongozi wa dini, serikali na kisiasa kushirikiana katika kuwachukulia hatua wale wote wanaofanya ukatili kwa wanawake wajawazito.

Halikadhalika Makamu wa Rais amewaasa watanzania kuachana na tabia za kuwapa msongo wa mawazo wanawake wajawazito kwani ni moja ya sababu zinazopelekea changamoto za uzazi ikiwemo kujifungua mtoto kabla ya wakati (njiti).

Ametoa rai kwa wadau mbalimbali nchini wakiwemo wanamuziki, wachezaji na hata waigizaji kuunga mkono jitihada za serikali katika kuokoa maisha ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti). Ameipongeza Taasisi ya Doris Mollel ambayo imekuwa ikitekeleza shughuli zake kwa takriban miaka nane sasa katika kusaidia Serikali kutoa huduma kwa watoto waliozaliwa kabla ya wakati na pia kusaidia katika utoaji wa vifaa tiba vinavyotumika kuokoa maisha ya watoto hao.

Aidha ameipongeza taasisi hiyo kwa kushirikiana na Oryx Energies Tanzania




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akimkabidhi mtungi wa gesi mwakilishi wa Mama wajawazito kutoka Wilaya ya Buhigwe Bi. Angel Leonce kwa lengo la kuhamasisha nishati safi ya kupikia pamoja na kukabiliana na changamoto zinazowakumba wajawazito. Mitungi hiyo imetolewa wakati wa hafla ya kupokea vifaa tiba vilivyotolewa na Taasisi ya Doris Mollel pamoja na vifaa tiba vilivyotolewa na Tume ya Ushindani (FCC) katika Hospitali ya Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma. Tarehe 06 Julai 2023.*

kujikita katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa akina mama wajawazito kwa kuwa tafiti zinaonesha mama mjamzito anayetumia nishati chafu katika kipindi cha ujauzito anakuwa yuko hatarini kupata mtoto njiti.

Amesema mpango huo ni muhimu kuwa endelevu kwani utatusaidia katika suala zima la kudhibiti uharibifu wa mazingira, ambao huchangiwa kwa kukata miti hovyo kwa ajili ya matumizi ya nishati. Ametoa rai kwa wananchi wa Buhigwe na maeneo mbalimbali nchini kuungana kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Ameishukuru Tume ya Ushindani (FCC) kwa kujitoa kuchangia huduma za afya ikiwemo utoaji wa dawa na vifaa tiba kwa Wana-Buhigwe kama sehemu ya kuchangia ustawi wa jamii ikiwa ni hatua ya kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha huduma za jamii hususan tiba kwa wazazi na watoto chini ya umri wa miaka mitano kama sehemu ya mkakati wa kupunguza vifo vya uzazi.

Makamu wa Rais ametoa wito wa kuongeza juhudi katika kuhamasisha, kukuza uelewa na kujenga uwezo wa jamii kuhusu lishe bora hususan kwa mama na mtoto. Amesema hilo ni jambo muhimu la kuzingatiwa ili kujenga afya njema ya akina mama wajawazito na hatimaye afya njema kwa watoto watakaozaliwa.

Dkt. Mpango amewapongeza mchezaji wa kimataifa Mbwana Samatta na Mwanamuziki wa kizazi kipya Ali Saleh Kiba maarufu kama Ali Kiba kwa kuanzisha taasisi yao na kucheza mechi za hisani ambazo zimekuwa moja ya nyenzo za kuchangia maendeleo hapa nchini ikiwemo kutoa vifaa tiba kwaajili ya kusaidia watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.

Kwa upande wake Mkurugenzi na Mwanzilishi wa Taasisi ya Doris Mollel, Bi Doris Mollel amesema Taasisi hiyo imekuwa ikishirikiana na serikali katika jitihada za kupunguza vifo vya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati pamoja na changamoto zinazopelekea kuzaliwa kwa watoto hao. Pia amesema taasisi hiyo imeshiriki katika kutoa vifaa tiba hapa nchini pamoja na utungaji sera za kukabiliana na ongezeko la watoto wanaozaliwa kabla ya wakati katika majukwaa mbalimbali ya kimataifa.

Bi. Mollel ameongeza kwamba taasisi imeendelea na jitihada za kuhakikisha marekebisho ya sheria ya likizo yanafanyika ili kuwapa muda wa miezi sita wakina mama wanaojifungua watoto kabla ya wakati kutokana na changamoto zinazowakumba.

Pia amesema tayari taasisi hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine wamefanikiwa kuhakikisha bima binafsi zinatoa huduma kwa mtoto anayezaliwa kabla ya wakati kupitia gharama ya bima ya mama wa mtoto.

Mwakilishi wa Tume ya Ushindani (FCC) Bi. Monica Moshi ambao wametoa vifaa tiba kwa Wilaya ya Buhigwe amesema utoaji wa vifaa tiba katika halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe ni sehemu ya kuchangia ustawi wa jamii jukumu ambalo wamekua wakitekeleza kila mwaka ikiwa ni hatua ya kuunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha huduma za tiba nchini hususani zile za uzazi na watoto chini ya miaka mitano ikienda sambamba na kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

# 'Wazazi, walezi simamieni vema watoto kupata elimu'




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwa darasani pamoja na viongozi mbalimbali mara baada ya kupokea Madarasa, Samani mbalimbali na Ofisi za Walimu yaliokarabatiwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) katika Shule ya Msingi Muyama iliopo Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma. Tarehe 05 Julai 2023.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanasimamia vema watoto wao kupata elimu kwa mustakbali wa Maisha yao na kuwa na uhakika wa wataalamu mbalimbali wa baadae kwa manufaa ya taifa.

Makamu wa Rais amesema hayo leo 05 Julai 2023 wakati aliposhiriki hafla ya kukabidhi madarasa matatu, ofisi mbili na samani katika shule ya Muyama iliopo Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma, madarasa yaliokarabatiwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB). Amesema serikali inaendelea na jitihada za kuboresha sekta ya elimu ikiwemo kuondoa ada kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha sita, kuongeza madarasa na shule ili kuwa na mazingira rafiki ya upatikanaji wa elimu.

Pia Makamu wa Rais amewaagiza wananchi, walimu na wanafunzi wa shule ya msingi Muyama kutunza vema majengo na samani katika shule hiyo ili viweze kutumika kwa muda mrefu. Amesema ukarabati wa majengo hayo unapaswa kwenda sambamba na utunzaji wa mazingira, ikiwa ni pamoja na usafi na upandaji miti ya aina mbalimbali kama vile ya matunda na kivuli. Halikadhalika ametoa wito kwa Halmashauri ya Buhigwe kwa kushirikiana na wadau wengine kufikiria kuanzisha mashindano ya kila mwaka ya usafi na uhifadhi wa mazingira katika Shule za Msingi na Sekondari.

Aidha Dkt. Mpango ametoa wito kwa wadau mbalimbali hapa nchini kujitokeza kuunga mkono juhudi za maendeleo ya jamii inayowazunguka hususan maeneo ya vijijini ambako mahitaji ni makubwa.

Katika hatua nyingine Makamu wa Rais ameahidi kuanzisha tuzo maalum zitakazoenda sambamba na zawadi kwa wanaofanya vizuri katika shule hiyo ya Msingi Muyama ambayo alipata elimu ya msingi mwaka 1968-1970 ili kuongeza ushindani na ari kwa walimu na wanafunzi wa shule hiyo.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa Shule ya Msingi Muyama mara baada ya hafla ya kupokea madarasa, samani mbalimbali na Ofisi za Walimu yaliokarabatiwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) katika Shule ya Msingi Muyama iliopo Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma 5, Julai 2023. (Wengine katika picha ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Prof. Joyce Ndalichako, Mkuu wa Mkoa Kigoma Thobias Andengenye, Mkurugenzi wa TCB Sabasaba Moshingi na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Muyama Stella Shayo)*



# Makamu wa Rais awaasa Watanzania kudumisha amani



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango pamoja na mkewe Mama Mbonimpaye Mpango wameungana na waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Yohane Bosco iliopo Miyuji jijini Dodoma katika Ibada ya Misa takatifu ya Jumapili ya Mwaka Mpya, Januaria 01, 2023, iliyoongozwa na Padre Innocent Nzavo.

Akizungumza mara baada ya ibada hiyo Makamu wa Rais amewaasa Watanzania kuendelea kudumisha amani hususani kwa kutenda haki katika familia ikiwemo kulinda haki za wanawake wanaokabiliwa na changamoto za ukatili.

Mhe. Dkt. Mpango amesema kuwa bado wanawake wanakabiliwa na dhuluma mbalimbali ikiwemo kupoteza mali pamoja na kunyimwa haki za ardhi.

Makamu wa Rais amesisitiza familia kuishi kwa amani katika mwaka 2023 ili kujiepusha na changamoto mbalimbali ikiwemo masuala ya ukatili. Amewasihi watanzania kuendelea kuliombea Taifa amani ili kila mmoja aweze kuishi salama.

Pia, ametoa wito kwa kwa waumini kujenga amani na mazingira ili kutokuharibu kwa utupaji taka ovyo pamoja na ukataji miti. Halikadhalika amewaasa watanzania kutumia wakati huu ambao mvua zimeanza kunyeesha kupanda miti katika maeneo yao.

Makamu wa Rais amewasihi viongozi wa dini na waumini kwa ujumla kuwaombea viongozi wa nchi ili waweze kuongoza vema kwa hekima ya Mungu na kwa maslahi ya taifa.



# Katibu Mkuu Maganga: Uhusiano wa Tanzania, Ujerumani umezaa matunda

*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akizungumza wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) Novemba 16, 2023 jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania Mhe. Thomas Terstegen pamoja na viongozi mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Wengine kuanzia kulia ni Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania Mhe. Thomas Terstegen, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango - Zanzibar Bw. Juma Malik Akil*

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga amesema kuwa uhusiano kati ya Tanzania na Ujerumani ni wa mfano kwani umeleta manufaa makubwa nchini.

Amesema hayo wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) Novemba 16, 2023 jijini Dodoma.

Bi. Maganga amesema kuwa kwa zaidi ya miaka 60, uhusiano baina ya nchi hizo mbili umezidi kuimarika kutokana na diplomasia iliyojengwa na viongozi wa nchi yetu kwa muda mrefu.



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akisalimiana na Kamishna Mkuu wa wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) Bw. Yusuph Mwenda wakati wa hafla ya chakula cha jioni na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) jijini Dodoma Novemba 16, 2023.*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akisikiliza maelezo kuhusu shughuli zinazofanywa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) wakati wa hafla ya chakula cha jioni jijini Dodoma Novemba 16, 2023. Wa pili kulia ni Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania Mhe. Thomas Terstegen.*

Amesema uhusiano huo umekuwa chachu ya ziara ya Rais wa Ujerumani Mhe. Frank-Walter Steinmeier aliyefanya ziara ya kikazi nchini Tanzania.

Ameishukuru Serikali ya Ujerumani kwa kushirikiana na Tanzania katika sekta mbalimbali kupitia miradi ikiwemo ya mabadiliko ya tabianchi na upatikanaji wa maji akisema kuwa, hiyo ni ajenda ya kidunia hivyo ni muhimu kukabiliana na athari zake.

Hali kadhalika ametoa shukrani na pongezi kwa Serikali ya Ujerumani kupitia GIZ Tanzania inavyoshiriki katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia ambao ni changamoto inayogusa baadhi ya maeneo nchini.

Kwa upande wake Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania Mhe. Thomas Terstegen ameshukuru na kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais Frank-Walter Steinmeier ambao wamefungua milango zaidi ya diplomasia kati ya nchi hizo mbili. Amesema kuwa miongoni mwa mambo aliyohimiza Rais Steinmeier wakati wa ziara yake nchini, ni wananchi kuchangamkia fursa za kiuchumi zinazopatikana ndani ya ushirikiano baina ya nchi hizo mbili.

Balozi huyo pia, amesema ni matumaini kuwa Ujerumani na Tanzania zitaendeleza ushirikiano wao ambao umedumu kwa zadi ya miaka 60.

Hafla hiyo imehudhuriwa na viongozi mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wakiwemo Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango - Zanzibar Bw. Juma Malik Akil na Mkurugenzi Mkazi wa GIZ Bw. Johanned Sperrfechter.



*Wageni mbalimbali wakiwa katika hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga jijini Dodoma Novemba 16, 2023.*

# Dkt. Jafo atoa wito ulinzi wa mazingira Ziwa Tanganyika




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akikabidhiwa zawadi na Mwenyekiti mpya wa Mkutano wa 11 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Ziwa Tanganyika (LTA) ambaye ni Waziri wa Uchumi wa Kijani na Mazingira wa Zambia Mhe. Mhandisi Dkt. Collins Nzovu mara baada ya mkutano huo uliofanyika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mulungushi Novemba 17, 2023 jijini Lusaka, Zambia.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo ametoa wito wa kulinda na kuhifadhi mazingira ya Ziwa Tanganyika na rasilimali zake ili liendelee kuinufaisha jamii na kuleta maendeleo endelevu.

Amesema ni wajibu wetu kuhakikisha changamoto zinazolikabili zikiwemo kupungua kwa kina cha maji, uchafuzi wa mazingira kutoka viwandani na majumbani, upotevu wa bioanuai na mchanga zinakwisha.

Dkt. Jafo ametoa wito huo wakati akifungua Mkutano wa 11 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Ziwa Tanganyika uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mulungushi jijini Lusaka, Zambia Novemba 17, 2023.

Dkt. Jafo amesema ziwa hilo ni urithi wa shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanywa ndani ya bonde zikiwemo uvuvi, kilimo, ufugaji, makazi ya watu na uchimbaji madini.

"Tutambue kuwa Ziwa Tanganyika ni zaidi ya kapu la chakula kwa jamii zetu na bonde lake ni nyumbani kwa zaidi ya watu milioni 13, ni eneo bora kwa kuunganisha nchi zetu nne zinazolizunguka, hivyo hatuna budi kushirikiana kwa pamoja katika uhifadhi na kuwezesha matumizi sahihi ya rasilimali zake," amesisitiza.

Aidha, Dkt. Jafo amesema kuwa mkutano huo ni muhimu katika kutathmini hatua iliyofikiwa kuelekea matumizi endelevu ya rasilimali na utekelezaji wa miradi chini ya mpango wa kikanda, hii ni fursa ya kutoa mwongozo kuelekea lengo hilo. Katika Mkutano huo tukio la kutia saini Itifaki ya Maendeleo ya Ufugaji wa Majini katika Ziwa Tanganyika na bonde lake lilifanyika.

Ameshukuru wadau wa maendeleo kwa juhudi zao katika usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika kupitia miradi wanayotekeleza na kusema kuwa Serikali ya Tanzania inalichukulia kwa uzito mkubwa suala la maendeleo endelevu



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa katika picha ya pamoja na Ujumbe kutoka Tanzania na wadau wa maendeleo mara baada ya kumalizika kwa Mkutano wa 11 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Ziwa Tanganyika uliofanyika jijini Lusaka, Zambia Novemba 17, 2023.*

ya Bonde la Ziwa Tanganyika.

Akifunga mkutano huo Dkt. Jafo amempongeza Waziri wa Uchumi wa Kijani na Mazingira wa Serikali ya Zambia Mhe. Mhandisi Dkt. Collins Nzovu kwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Baraza Kuu la Mawaziri.

Katika mkutano huo, washiriki wamepokea na kujadili masuala mbalimbali muhimu yakiwemo taarifa za uchambuzi wa uwezekano wa kuwajumuisha Makatibu Wakuu katika Vyombo vya Sheria vya LTA, Itifaki ya Maendeleo ya Kilimo cha Majini kwa Ziwa Tanganyika na bonde lake;.

Taarifa zingine ni utafiti kuhusu maeneo muhimu ya bioanuai katika Ziwa Tanganyika na bonde lake, hali ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, hali ya michango ya kitaifa na mpango kazi wa mwaka na bajeti ya LTA ya mwaka 2024.

> **Tutambue kuwa Ziwa Tanganyika ni zaidi ya kapu la chakula kwa jamii zetu na bonde lake ni nyumbani kwa zaidi ya watu milioni 13, ni eneo bora kwa kuunganisha nchi zetu nne zinazolizunguka, hivyo hatuna budi kushirikiana kwa pamoja katika uhifadhi na matumizi sahihi ya rasilimali zake**

Mkutano huo umehudhuriwa pia na Waziri wa Mazingira, Kilimo na Mifugo wa Burundi ambaye ni mwenyekiti anayemaliza muda wake Mhe. Mhandisi Prosper Dodiko, Waziri wa Uvuvi na mifugo wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Mhe. Adrien Bokele Djema na Mkurugenzi Mtendaji wa LTA Sylvain Tusanga Mukanga.

Ujumbe ulioshiriki katika Mkutano huo uliwashirikisha pia Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi, Mkurugenzi wa Mazingira Bi. Kemilembe Mutasa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira Dkt. Deogratius Paul.

Baraza hilo linaundwa na Mawaziri kutoka nchi nne ambazo ni Tanzania, Zambia, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akifanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Shirika la Mazingira la Korea (KEPO) Dkt. Yoon, Young-bong jijini Incheon, Korea Kusini kuhusu ushirikiano katika teknolojia ya usimamizi wa taka. Kushoto ni Balozi wa Tanzania nchini Korea Kusini Mhe. Togolani Mavura.*

# Dkt. Jafo akaribisha Shirika la Mazingira Korea kuwekeza teknolojia usimamizi taka

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Shirika la Mazingira la Korea (KEPO) Dkt. Yoon, Young-bong jijini Incheon, Korea Kusini Oktoba 28, 2023.

Katika mazungumzo yao Dkt. Jafo ameeleza nia ya Tanzania katika kuanzisha ushirikiano kwenye sekta ya utunzaji wa mazingira hususani katika teknolojia ya usimamizi wa taka.

Katika kikao hicho akiwa na Balozi wa Tanzania nchini Korea Kusini Mhe. Togolani Mavura, viongozi hao wamejadili kuhusu kubadilishana uzoefu wa kisera katika upande wa mazingira.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa shirika hilo Dkt. Young-bong amemueleza Waziri Dkt. Jafo kuwa wako tayari kushirikiana na Tanzania katika usimamizi wa taka.

Hivyo, viongozi hao wamekubaliana kuendeleza mazungumzo katika kuelekea hatua za utekelezaji wa ushirikiano huo ambao unatarajiwa kusaidia katika utunzaji wa mazingira nchini Tanzania.

Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imeendelea kuibua miradi ya kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia taka nchini Tanzania.

Amesema Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Mpango Kabambe wa Hifadhi ya Mazingira (2022 – 2032) ambao pamoja na mambo mengine changamoto za hifadhi ya mazingira na hatua za kukabiliana nazo zimeainishwa. Hali kadhalika Ofisi kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mwongozo wa Usimamizi Endelevu wa Taka kwa kuzingatia dhana ya 'Punguza Uzalishaji wa Taka, Tumia tena na Rejeleza'.

Katika ziara hiyo ya kikazi ya kuimarisha ushirikiano katika masuala ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Waziri Dkt. Jafo ameambatana na Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Dustan Shimbo.

Itakumbukwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuimarisha diplomasia na mataifa mbalimbali duniani.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Shirika la Mazingira la Korea (KEPO) Dkt. Yoon, Young-bong mara baada kikao kilichofanyika jijini Incheon, Korea Kusini.*

# Serikali kuimarisha usimamizi rasilimali kuongeza wigo wa kunufaisha jamii

Serikali imesema itaendelea kuimarisha sera, mipango na mikakati ya usimamizi wa rasilimali za bahari na kuongeza wigo wa manufaa ya kijamii na kiuchumi baina ya nchi wanachama zinazotekeleza Mkataba wa Nairobi.

Rai hiyo imetolewa jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga wakati akifungua Warsha ya Kikanda kuhusu Mpango wa Matumizi ya Eneo la Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi mwa Bahari ya Hindi iliyoshirikisha nchi 10 zinazotekeleza Mkataba wa Nairobi unaohusu Hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi.

Bi. Maganga amesema lengo la warsha hiyo ni kujenga uwezo wa wataalamu kutoka nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi katika kuandaa na kutekeleza Mpango wa Matumizi ya eneo la Bahari, Usimamizi wa taarifa za kimazingira, kubadilishana uzoefu na kufahamu hatua zilizofikiwa na nchi wanachama katika kuandaa na kutekeleza mpango wa Matumizi ya eneo la Bahari.




*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akifurahia jambo na wajumbe wa warsha ya Mafunzo ya Kikanda kuhusu Mpango wa Matumizi ya Eneo la Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi mwa Bahari ya Hindi iliyofanyika jijini Dar es Salaam.*



Amesema warsha hiyo inasaidia kuandaa mpango na usimamizi endelevu wa matumizi ya rasilimali za bahari ikiwa ni pamoja na mgawanyo sahihi wa matumizi ya bahari na kuongeza kuwa Tanzania imejipanga kikamilifu ambapo imendaa mpango huo kwa kuzingatia kuwa uchumi wa buluu ni miongoni mwa agenda za dunia.

"Ninapozungumzia uchumi wa bluu ninasisitiza usimamizi endelevu na shirikishi wa mifumo ikolojia ya Pwani na bahari ya Tanzania ili kuendelea kutoa bidhaa na huduma muhimu ikiwa ni pamoja masuala ya uvuvi na uchimbaji wa mafuta na gesi pale vitakakapogundulika," amesema Bi. Maganga.

Akifafanua zaidi amezitaja nchi zinazotekeleza Mkataba wa Nairobi kuwa ni pamoja na Tanzania, Comoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Shelisheli, Re-Union na Afrika Kusini ambapo kupitia warsha hiyo wataalamu wa mataifa hayo watajadili ajenda mbalimbali za mazingira na jitihada zinazopaswa kuchukuliwa na nchi wanachama.

Kwa upande wake, Mratibu kutoka sekretarieti ya Mkataba huo, Bw. Dixon Waruinge amesema nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi hazina budi kuwa na mkakati wa pamoja wa usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za bahari katika ukanda wa bahari ya Hindi kwa kuwa ni moja ya hatua muhimu ya kukabiliana na majanga mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi.

"Sote ni mashahidi kwa kile kilichotokea kwa nchi za Msumbiji, Malawi na Madagascar ambazo zilikabiliwa na kimbunga cha Freddy ambacho kilileta madhara mbalimbali ikiwemo vifo vya binadamu na viumbe hai wengine-Juhudi za pamoja ni muhimu katika kuimarisha hifadhi za bahari," amesema Waruinge.

Nae Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira Asili ya Dunia (IUCN) Bi. Minna Epps amesema jitihada za pamoja baina ya wadau wa mazingira bado zinahitaji katika kuhakikisha nchi zote zinaendelea kuweka mkazo katika uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari kuokoa uhai wa rasilimali zilizopo.



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis akiwapa chakula samaki wanaofugwa na kikundi cha vijana cha INAWEZEKANA, Kata ya Lugarawa kilichonufaika na Mradi wa Kuhifadhi Ardhi (SLM) katika Bonde la Ziwa Nyasa wilayani ya Ludewa mkoani Njombe unaotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.*

# Naibu Waziri Khamis awataka wananchi kutunza vyanzo vya maji

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis amewataka wananchi kutunza vyanzo vya maji ili viwanufaishe na kuhifadhi mazingira.

Amesema hayo wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua Mradi wa Kuhifadhi Ardhi (SLM) katika Bonde la Ziwa Nyasa wilayani ya Ludewa mkoani Njombe Oktoba 18, 2023.

Mhe. Khamis amesema shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zinazofanyika kupitia mradi huo zikiwemo ufugaji wa samaki ni matunda ya uwepo wa vyanzo vya maji

Amesema Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa maeneo yenye vyanzo vingi vya maji hivyo ametoa rai kwa viongozi kuhakikisha vyanzo hivyo vinatunzwa.

"Ndugu zangu Mwenge wa Uhuru si umepita huku kwenu?..Na mmeona ujumbe wake ulihimiza namna ya kutunza mazingira na kuhifadhi vyanzo vya maji sasa leo hii yale mabwawa ya samaki yasingekuwepo kama tusingekuwa na vyanzo vya maji, leo hii nimepita kule nimeona mnafanya kilimo cha umwagiliaji yanafanyika haya kwa sababua tuna vyanzo vya maji, tuvitunze" amesisitiza.

Naibu Waziri Khamis amewataka wananchi kuwa walinzi wa vyanzo vya maji vitunze ili wanufaike kinyume na hapo watakuwa wanategemea tu mvua inyeshe ndipo wapate maji.

Sanjari na vyanzo vya maji, pia Mhe. Khamis amewataka wananchi kuitunza miradi hiyo walioyonufaika nayo ikiwemo kupanda miti kwa wingi ili iwanufaishe.

Amewatahadharisha wananchi kulinda amani iliyopo kuepuka madhara yanatokana na migogoro mbalimbali inayoweza kujitokeza endapo amani itachezewa.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Lugarawa Mhe. Erasto Mhagama akizungumzia mradi wa ufugaji wa samaki unaotekelezwa kupitia SLM katika kata hiyo ameshukuru Serikali kwa kuwapelekea mradi huo katika wilaya yao.

Ameiomba Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais inayotekeleza mradi huo chini ya ufadhili wa Mfuko Mazingira wa Dunia (GEF) kuongeza wigo wa utekelezaji wa mradi ili uwafikie wananchi wengi zaidi.

Nae Bw. Longinus Mgani ambaye ni mwenyekiti wa Kikundi cha INAWEZEKANA kinachojishughulisha na mradi wa ufugaji wa samaki amesema wameitumia fursa ya mradi kujikwamua kimapato.

Amesema kuwa mradi huo umewapa hamasa ya kuacha kufanya shughulli za kilimo cha kuhamahama kisicho endelevu na kukata miti ambazo husababisha uharibifu wa mazingira.

Mradi wa Kuhifadhi Ardhi (SLM) katika Bonde la Ziwa Nyasa unatekelezwa katika halmashauri za wilaya tano zikiwemo ya Kyela (Mbeya), Makete na Ludewa (Njombe), Mbinga na Nyasa (Ruvuma).

Lengo la mradi, pamoja na kuhifadhi ardhi katika eneo hilo ni kuisaidia jamii kufanya shughuli za kujipatia kipato bila kuathiri mazingira na kulinda hifadhi ya Bonde la Ziwa Nyasa.



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis vifaranga vya kuku kwa kikundi cha akinamama katika Kijiji cha Mdildili Kata ya Lugarawa wakati alipofanya ziara ya kwenye ziara ya kikazi ya kukagua Mradi wa Kuhifadhi Ardhi (SLM) katika Bonde la Ziwa Nyasa wilayani ya Ludewa mkoani Mbeya unaotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.*

# Dkt. Jafo: Biashara ya Kaboni inachangamkiwa sana



*Waziri Dkt. Selemani Jafo*



*Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria Ofisi ya Makamu wa Rais, Bwana Dustan Shimbo*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Ufuatiliaji wa Kaboni (NCMC) Prof. Eliakimu Zahabu*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amesema mwitikio wa uwekezaji wa Biashara ya Kaboni umezidi kuongezeka kutokana na mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyofanywa na Serikali.

Amesema hadi sasa kampuni 34 tayari zimesajiliwa na kusisitiza kuwa milango ya uwekezaji wa biashara hiyo ipo wazi huku akisisitiza Serikali inaendelea kuwakaribisha na kuwaunga mkono wawekezaji wote.

Dkt. Jafo amesema hayo alipokutana na kuzungumza na wadau wa Biashara ya Kaboni jijini Dar es Salaam Novemba 23, 2023 ambapo amemuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Ufuatiliaji wa Kaboni (NCMC) Prof. Eliakimu Zahabu kuhakikisha wanatatua haraka changamoto zinazojitokeza katika usajili wa biashara hiyo.

Amesema ni vyema kuona vijana wakinufaika na biashara ya kaboni kwa kupata na wakati huo Serikali ikipata mapato pamoja na mazingira kuwa salama zaidi kwa kuwa kila mtu atalinda cha kwake.

“Serikali ipo nanyi kuwasiiliza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan anawategemea sana katika ajenda yake hii ya biashara ya kaboni ndio maana mikutano yake yote anazungumzia biashara hii, hivyo tuisaidie nchi kwani utajiri tuliokuwa nao tukiutumia vizuri nchi yetu itakuwa ya mfano,” amesema Dkt. Jafo.

Kwa upande wake Prof. Zahabu amesema kituo hicho kimekuwa na uwazi na wakati huo kipo kuwezesha mchakato kwa kila mtu anayehitaji kufanya usajili au huduma yoyote kuhusiani na kaboni.





*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Bw. Abdallah Hassan Mitawi akizungumza jambo wakati wa ufunguzi wa warsha ya mafunzo kwa Maafisa ununuzi wa Wizara za Serikali ya MaPinduzi Zanzibar kuhusu udhibiti wa uingizaji wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal Septemba 26, 2026, Zanzibar. Kulia ni Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar. Bi Farhat Ali Mbarouk na kushoto ni Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na (Mazingira) Mhandisi Catherine Bamwenzaki.*

# Mitawi: Maafisa Ununuzi zingatieni miongozo ya ununuzi wa vifaa

Maafisa Ununuzi wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wametakiwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo wakati wa ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vyenye kemikali zilizowekewa ukomo wa matumizi ili kuzuia athari uharibifu wa mazingira na kulinda afya za binadamu.

Rai hiyo imetolewa Septemba 26, 2023 Zanzibar na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Bw. Abdalllah Haasn Mitawi wakati akifungua warsha ya mafunzo kwa Maafisa Ununuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu udhibiti wa uingizaji wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal.

Kwa mujibu wa Mitawi amesema asilimia kubwa ya bajeti ya Serikali imeelekezwa katika eneo la ununuzi wa vifaa na vitendea kazi mbalimbali katika ofisi za umma, hivyo ni wajibu wa maafisa manunuzi kuhakikisha wanazingatia miongozo iliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria ili kuepusha hasara kwa serikali na kulinda afya kwa binadamu na mazingira.

> **Maofisi yote ya umma tunatumia viyoyozi na majokozi kama sehemu ya kupata hewa safi...Maafisa ununuzi ndio mnahusika moja kwa moja katika ununuzi wa vitendea kazi hivi...Tunapaswa kufahamu kuwa kunaaina fulani ya kemikali zilizopo katika vitendea kazi hivi zina athari kwa mazingira yetu....kupitia mafunzo haya mtaweza kufahamishwa**

"Maofisi yote ya umma tunatumia viyoyozi na majokozi kama sehemu ya kupata hewa safi...Maafisa ununuzi ndio mnahusika moja kwa moja katika ununuzi wa vitendea kazi hivi...Tunapaswa kufahamu kuwa kunaaina fulani ya kemikali zilizopo katika vitendea kazi hivi zina athari kwa mazingira yetu....kupitia mafunzo haya mtaweza kufahamishwa" amesema Mitawi

Mitawi amesema kwa mujibu kwa Itifaki ya Montreal ambapo Tanzania iliridhia mkataba huo mwaka 1993, nchi zote 197 zimekubaliana kutotumia kemikali zilizodhibitiwa kupitia ili kulinda Tabaka la ozoni kwa kuwa hatua hiyo itasaidia juhudi za ulimwengu kuepuka athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ongezeko la joto, ukame na vifo vya binadamu, wanyama na mifugo.

Akifafanua zaidi Mitawi amesema maafisa ununuzi na ugavi wana nafasi kubwa ya kuisadia Serikali na jamii kwa ujumla kuhusu udhibiti wa kemikali zilizodhibitiwa kwa mujibu wa itifaki ya Montreal ambapo kwa



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Bw. Abdallah Hassan Mitawi akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa mafunzo kwa kwa Maafisa ununuzi wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu udhibiti wa uingizaji wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal Septemba 26, 2026, Zanzibar.*

kutambua umuhimu huo, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa imeendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa wa kada hiyo.

"Baada ya mafunzo haya mtapokuwa maofisi...Hakikisheni pale ambapo Katibu Mkuu au Afisa Masuhuli akihitaji kufanya manunuzi ya viyoyozi au majokofu...ni wajibu wenu kuhakikisha tunatoa ushauri wa kitaalamu kama ambavyo tutaelekezwa na wakufunzi kupitia mafunzo haya" amesema Mitawi.

Mitawi amesema dunia kwa sasa imeshuhudia kiwango kikubwa cha athari za mabadiliko ya tabia ikiwemo ongezeko la joto katika maeneo mbalimbali, magonjwa, mvua zisizotabirika na ukame uliokithiri unaotokana matendo unaofanywa na binadamu ikiwemo uharibifu wa tabaka la ozoni.

"Sote ni mashahidi kwa yanayotokea kwa sasa huko Ulaya.... Tunaelezwa na wanahistoria kuwa dunia imekabiliwa na kiwango kikubwa cha joto kuwahi kutokea..... Mafunzo yana umuhimu mkubwa kwetu katika kutambua aina ya vifaa vyenye kemikali vinavyonunuliwa katika Ofisi zetu vimezingatia Itifaki ya Montreal ili kunusuru afya za binadamu na mazingira" amesema Mitawi.

> **Asilimia kubwa ya kemikali hizi tumekuwa tukizinunua kutoka nje ya nchi...hivyo tukiwa kama Maafisa Ununuzi tunapaswa kuwa mstari wa mbele tunatoa ushauri wa kitaalamu na elekezi katika ununuzi wa vifaa na vitendea kazi ili uharibifu wa tabaka la ozoni**

Mitawi amesema Tanzania kama nchi imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kukabiliana athari za mabadiliko ya tabianchi yenye lengo la kudhibiti uingizaji na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa kemikali zinazodhibitiwa kwa kushirikiana na ili kuzuia madhara mbalimbali kwa jamii ikiwemo magonjwa, ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Catherine Bamwenzaki amesema asilimia kubwa ya kemikali zinazoharibu tabaka la ozone zimekuwa zikiagizwa kutoka nje ya nchi, hivyo ili kujenga uelewa wa pamoja Serikali imeendelea kutoa elimu na mafunzo kwa makundi mbalimbali katika jamii.

"Asilimia kubwa ya kemikali hizi tumekuwa tukizinunua kutoka nje ya nchi...hivyo tukiwa kama Maafisa Ununuzi tunapaswa kuwa mstari wa mbele tunatoa ushauri wa kitaalamu na elekezi katika ununuzi wa vifaa na vitendea kazi ili uharibifu wa tabaka la ozoni" amesema Mhandisi Bamwenzaki.

Naye Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar. Bi Farhat Ali Mbarouk ameishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yataongeza tija na ufanisi kwa Maafisa ununuzi wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

"Mafunzo kwa maafisa ununuzi wa Wizara za SMZ zitaongeza tija kwa watendaji wetu katika katika kutambua vifaa na vitendea kazi vyenye kemikali zenye ukomo wa matumizi" amesema Farhat.

# Tanzania yapokea shilling bilioni 7.3 kukabili mabadiliko ya tabianchi

Serikali ya Tanzania imenufaika na shilingi bilioni 7.3 kutoka Serikali ya Norway kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na inayotekelezwa nchini.

Hayo yamejiri baada ya Serikali hizo mbili kusaini Makubaliano ya kushirikiana katika shughuli za mazingira, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam Septemba 07, 2023.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo kwa niaba ya Serikali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amesema Tanzania itajengewa uwezo katika utekelezaji wa shughuli za mazingira.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo na Waziri anayeshughulikia masuala ya Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa na nchi za Nordic Mhe. Anne Beathe Tvinnereim wakisaini makubaliano ya ushirikiani kati ya Serikali ya Tanzania na Norway kuhusu ushirikiano katika hifadhi ya mazingira jijini Dar es Salaam Septemba 07, 2023. Anayeshuhudia ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Dustan Shimbo.*



*Balozi wa Norway nchini Tanzania Bi. Tonne Tinnes na Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Maendeleo (UNFCC) Bw. Peter Malika wakisaini makubaliano ya kushirikiana ya kiasi cha shilingi bilioni 7.3 kwa ajili ya kusaidia wilaya za Mkoa wa Dodoma katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.*

Alisema makubaliano hayo ni chachu katika kuijengea Tanzania kuweza kunuifaika na fedha za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kutoka nchi zilizoendelea ambazo ziliahidi.

Dkt. Jafo alifafanua kuwa makubaliano hayo ni mwendelezo wa makubaliano yaliyosainiwa mwaka 2022 katika Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 27) uliofanyika Sharm El Sheikh nchini Misri ambayo yalijikita katika kupunguza hewa chafu.

Pia, alisema Norway imeiunga mkono Tanzania katika mikakati yake ikiwemo kupunguza gesi joto, utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2022 hadi 2032 pamoja Sera ya Uchumi wa Bluu.

"Makubaliano tuliyosaini yatasaidia katika miradi yetu ya kimazingira katika sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, nishati, maji, afya na ardhi na tuishukuru sana Serikali ya Norway, na sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais tunafurahi sana kwa miradi hii ambayo inakwenda kutatua changamoto za mabadiliko ya tabianchi," alisema Dkt. Jafo. Kwa upande wake Waziri anayeshughulikia masuala ya Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa na nchi za Nordic Mhe. Anne Beathe Tvinnereim aliyesaini kwa niaba ya Serikali ya Norway alisema kuwa makubaliano hayo ni matunda ya uhusiano wa muda mrefu wa Serikali hizo mbili.

Alisema nchi yake imejipanga katika kuyatendea haki makubaliano hayo kwa kuelekeza miradi hiyo kwa wananchi wanaokabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yao.

Mhe. Anne alisema kuwa Serikali ya Norway kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imepanga kufanya utafiti kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa Biashara ya Kaboni ambayo imeshika kasi hapa nchini.

Naye Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Maendeleo (UNFCC) Tanzania Bw. Peter Malika alisema fedha hizo zilizotolewa zitasambazwa katika wilaya sita za Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kusaidia miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Alisema pia kutakuwa na mafunzo kwa jamii zilizoathirika na mabadiliko ya tabianchi kuhusu namna ya kutambua changamoto hizo kwa ajili ya mikakati ya kuanzisha miradi.

Aprili 21, 2008 nchi hizo mbili zilisaini makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi hatua iliyoanzisha Kituo cha Taifa cha Kufuatilia Kaboni (NCMC).




*Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi akifungua Semina ya Uchumi wa Buluu na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Wizara za kisekta Oktoba 17, 2023 jijini Dodoma. Kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango Bw. Ignas Chuwa na Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Bi. Kemilembe Mutasa.*

# Mitawi: Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu yakaribia kuiva

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kutunga Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu na Mkakati wake wa utekelezaji kwa lengo la kuweka mfumo jumuishi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali zake ili kukuza uchumi wa nchi na maendeleo endelevu.

Hayo yamebainishwa na Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi wakati wa Ufunguzi wa Semina ya Uchumi wa Buluu na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Wizara za kisekta Oktoba 17, 2023 jijini Dodoma.

Amesema Uchumi wa Buluu ni dhana ambayo inachagiza ukuaji wa uchumi kupitia matumizi endelevu ya rasilimali maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa jamii.

Bw. Mitawi mafunzo hayo yatawajengea uwezo washiriki kuhusu jinsi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia programu ya Msaada wa Kibajeti pamoja na Kukuza na kuongeza ujuzi katika masuala ya uchumi wa buluu na mabadiliko ya tabianchi.

"Sote tunatambua kwamba mabadiliko ya tabianchi yapo na ni ya kweli na tayari athari zake zimeshaanza kuonekana na zimeleta madhara makubwa katika maeneo ya bahari na mito nchini kama tunavyoshuhudia vimbunga, El-Nino pamoja na kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari na mito," amesema Mitawi.

Hivyo, kwa muktadha huo ametoa wito wa kuchukua kukabiliana na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kulinda na kuhifadhi Misitu yetu, vyanzo vya maji na rasilimali zote ambazo ndio tegemeo katika nyanja ya Uchumi wa Buluu.

Aidha, ameishukuru Jumuia ya Ulaya kwa kusaidia Serikali kutekeleza shughuli zenye mnasaba na uchumi wa buluu ili kujenga uchumi imara na endelevu kupitia shughuli za uchumi buluu.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Kemilembe Mutasa amesema semina hiyo ya siku mbili mbali ya kuwashirikisha wataalamu kutoka Tanzania Bara pia itawafikia Tanzania Zanzibar.

Amesema masuala ya mabadiliko ya tabianchi ni eneo lenye changamoto hivyo Tanzania imekuwa na programu mbalimbali inazotekeleza kama nchi mwanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi.



*Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Semina ya Uchumi wa Buluu na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Wizara za kisekta Oktoba 17, 2023 jijini Dodoma.*



*Waziri Mkuu Mstaafu, Mhe. Mizengo Pinda akisaini kitabu cha wageni muda mfupi baada ya kuwasili katika Banda la Ofisi ya Makamu wa Rais iliyoshiriki Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 07, 2023.*

# Pinda atoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kutangaza fursa za Biashara ya Kaboni

Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda ametoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kutangaza fursa za Biashara ya Kaboni ili kuwawezesha wananchi kupata mwako wa kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti hivyo kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ametoa rai hiyo wakati alipotembelea banda la Ofisi ya Makamu wa Rais wakati wa Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 7, 2023.

Mhe. Pinda amesema biashara ya kaboni inahusisha zaidi upandaji na utunzaji wa miti na kuweka mifumo inayodhibiti uzalishaji wa hewa ukaa katika shughuli mbalimbali ikiwemo za kilimo, nishati, viwanda, na miundombinu hivyo ni wajibu wa elimu ya biashara hiyo iendelee kutolewa katika Mikoa yote nchini.

"Biashara hii imeingia katika Mkoa wa Katavi na tayari wananchi wamenufaika na mradi huu kwa kuongeza mapato na kuimarisha utoaji wa huduma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa sambamba na kuzuia uharibifu wa misitu iliyohifadhiwa," amesema Mhe. Pinda

Kwa mujibu wa Pinda, elimu ya kutosha ikitolewa kwa wananchi kuhusu fursa ya biashara hiyo jitihada hizo zitawawezesha wananchi kupata uelewa na kunufaika na biashara hiyo wakiwemo wakulima na wafugaji.

Akifafanua zaidi Mhe. Pinda amesema kazi kubwa iliyopo kwa sasa ni kuhamasisha wananchi kuhifadhi misitu ya asili na kutunza mazingira kwa kuhakikisha hakuna ukataji miti hovyo, uchomaji misitu na kuzuia kufanyika kwa shughuli zingine hatarishi.

Kwa upande wake Afisa Mazingira Mwandamizi Ofisi ya Makamu wa Rais, Abdallah Lungo amesema kwa kutambua umuhimu wa biashara hiyo, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeanza kufanyia maboresho Ka-



*Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda akitazama kitabu cha Muungano kilichoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais wakati alipotembelea Banda la Ofisi hiyo iliyoshiriki Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 07, 2023.*



*Waziri Mkuu Mstaafu, Mhe. Mizengo Pinda akipokea machapisho mbalimbali yanatolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Hanifa Selengu muda mfupi baada ya kutembelea Banda la Ofisi hiyo iliyoshiriki Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 07, 2023.*




*Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasimaliwatu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Bw. Elisha Msengi akibadilishana mawazo na Katibu Mkuu mstaafu na Mjumbe wa Baraza la Kumshauri Rais kuhusu utekelezaji wa masuala ya Kilimo na Chakula Dkt. Frolence Turuka wakati wa ziara iliyofanywa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mhe. Mizengo Pinda katika Banda la Ofisi ya Makamu wa Rais iliyoshiriki Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) Kitaifa katika Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 07, 2023.*

nuni na Mwongozo wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2022 ili ziweze kuwatambua na kuwanufaisha wakulima na wafugaji nchini.

Aidha Lungo amesema kuandaliwa kwa kanuni na mwongozo wa biashara hiyo, kutawezesha kuuzwa kwa wingi hewa ya ukaa na ukamilifu wake na kuwezesha misitu iliyopo katika vijiji husika kulipwa kiasi kikubwa cha fedha na hivyo Serikali inaendelea kuwahimiza wananchi kuhifadhi misitu na kutunza mazingira.

"Matumizi bora ya ardhi ndio chanzo cha biashara hii kwa maana ya kutenga maeneo ya hifadhi ya misitu na kuilinda. Tumeendelea kuhimiza jamii kutunza mazingira kwa kupanda miti kwa ajili matumizi mbalimbali sambamba na kufyonza hewa ukaa kwa manufaa endelevu" amesema Lungo. Katika ziara hiyo, Mhe. Pinda aliongozana na Viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Rukwa akiwemo Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Makongoro Nyerere na Katibu Tawala Bw. Gerald Kusaya.

Ofisi ya Makamu wa Rais imeungana na Wizara, Idara na Taasisi za Umma na binafsi kushiriki Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) mwaka 2023 yaliyoongozwa na kauli mbiu isemayo "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifuko ya Chakula."




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akifungua Maonesho ya Kitaifa ya Kilimo ya Nane nane yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya Agosti 01, 2023. Wengine kuanzia kulia ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya Dkt. Stephen Mwakajumilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Juma Homera, Mke wa Makamu wa Rais Mama Mbonimpaye Mpango Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, Spik awa Bunge Dkt. Tulia Ackson na aliyekuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi David Silinde.*

# Makamu wa Rais akemea wavamizi maeneo ya utafiti wa kilimo

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amekemea tabia ya uvamizi na mtindo wa kubadili matumizi ya ardhi iliyotengwa mahsusi kwa ajili ya Utafiti wa Kilimo.

Makamu wa Rais ametoa maagizo hayo Agosti 01, 2023 wakati akifungua maonesho ya Nanenane kitaifa yanayofanyika katika viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya. Amesema maeneo mengi ya taasisi za utafiti yamevamiwa na kupimwa viwanja jambo ambalo linatishia utafiti wa kilimo na mifugo kwa kuwa vituo vya utafiti vitakosa maeneo ya kutosha ya kufanyia kazi.

Amewataka watanzania kutambua kilimo ni sayansi na hivyo utafiti kilimo usipopewa kipaumbele basi mapinduzi ya kilimo yatabaki kuwa ndoto. Amesisitiza umuhimu wa kupima maeneo ya taasisi za utafiti wa kilimo, kupewa hati na kulindwa wakati wote. Vivyo hivyo ameelekeza mamlaka zinazohusika kutenga na kupima ardhi katika maeneo ya uzalishaji wa mbegu na kuyalinda dhidi ya uvamizi.

Vilevile, Makamu wa Rais amekemea uwepo wa makundi makubwa ya mifugo yalioingizwa katika mikoa ya nyanda za juu kusini. Amesema madhara yake ni makubwa ikiwemo kuharibiwa sana kwa mazingira kuongezeka kwa migororo mingi kati ya wakulima na wafugaji, wanyama kama Tembo kukimbia bugudha ya mifugo na kuhamia kwenye makazi ya binadamu wakiharibu mazao na hata kuua watu. Amezitaka Wizara zote husika na Wakuu wa Mikoa kuchukua hatua thabiti kudhibiti uingizaji mifugo kinyemela katika maeneo yao ya utawala.

Makamu wa Rais ametoa wito kwa wakulima, wafugaji na wavuvi kuzingatia maelekezo ya wataalam ili kuweza kuzalisha pasipo kuathiri afya ya binadamu na mazingira kutokana na kuongezeka kwa matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu na kemikali nyingine jambo lenye athari kubwa kwa afya ya binadamu na viumbe hai vingine.

Ameongeza kwamba Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji nchini ikiwemo kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji, ambapo lengo ni kufikia eneo la umwagiliaji la hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025. Pia




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Asas Bw. Ahmed Asas alipotembelea banda la kampuni hiyo inayojishughulishaji na ufugaji wakati wa ufunguzi wa Maonesho ya Kitaifa ya Kilimo ya Nanenane Agosti 01, 2023 yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akisikiliza maelezo kutoka kwa Waziri wa Kilimo Hussein Bashe wakati alipotembelea banda la kilimo mara baada ya kufungua Maonesho ya Kitaifa ya Kilimo ya Nanenane leo tarehe Agosti 01, 2023 yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.*

ametoa wito kwa wananchi kutumia na kutunza miundombinu hiyo ili iweze kutumika kwa muda mrefu na kusaidia kuleta tija.

Makamu wa Rais ametoa rai kwa wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula ili taifa liweze kujitosheleza kwa chakula na kupata fedha zaidi za kigeni kutokana na mazao mbalimbali. Amasema Serikali kwa upande wake itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa kuwapatia Maafisa Ugani vitendea kazi mbalimbali vikiwemo pikipiki, vifaa vya matibabu, uhimilishaji pamoja na vifaa vya kupima afya ya udongo.

Ameitaka Wizara ya Kilimo na Mifugo kuanza maandalizi ya kuchukua vijana wengine katika programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (Building a Better Tomorrow - BBT) pamoja na kuziagiza Wizara za Kilimo na Mifugo na Uvuvi kuona namna bora ya kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili vijana wa JKT wanaojitolea wapewe kipaumbele kushiriki katika programu hiyo.

Makamu wa Rais ameendelea kusisitiza taasisi za fedha na mabenki hapa nchini kuendelea kushusha riba zaidi ili kuwasaidia wakulima na wafugaji. Ameitaka Wizara ya Kilimo na Fedha kufikiria kuanzishwa kwa mfuko wa maendeleo ya kilimo utakaosaidia kushusha riba kwa wakulima, wafugaji na wavuvi.

Amewapongeza watafiti waliosaidia katika upatikanaji wa mbegu na kutoa wito kwa Wizara ya Kilimo kutafuta utaratibu wa kuwapa tuzo vijana na wabunifu wanaotoa suluhu ya mambo mbalimbali katika kilimo, ufugaji na uvuvi.

Kwa upande wake Waziri wa Kilimo Hussein Bashe amesema sekta ya kilimo inaendelea kuimarika kutokana na juhudi za serikali katika kuinua sekta hiyo ikiwemo kuongezeka kwa bajeti kufikia shilingi bilioni 970 kutoka bilioni 294. Ameongeza kwamba kuimarika kwa sekta hiyo kumepelekea kuzalishwa kwa kahawa tani 80000, tumbaku kilo milioni 120 huku uzalishaji wa pamba ukiongezeka mara mbili. Bashe ameishukuru serikali kwa kutoa shilingi bilioni 100 ili kusaidia makampuni ya pamba yaweze kununua zao hilo kwa wakulima.

Waziri Bashe amesema maendeleo ya kilimo yanategemea ufanisi katika sekta zingine ikiwemo bandari. Ameongeza kwamba mabadiliko na uwekezaji wa tija katika bandari yanahitajika kwa sasa kwani yatasaidia wakulima katika kusafirisha mazao yao.

Pia amesema kuanzia mwaka 2024 nchi zote za Afrika zitapata mialiko ya kuhudhuria maonesho ya Nane nane huku akisisitiza mialiko hiyo haitahusisha viongozi pekee bali hadi wakulima na wanunuzi wa mazao wa nchi hizo. Ameongeza kwamba kufuatia kupanda hadhi kwa maonesho hayo kuwa ya kimataifa, juhudi mbalimbali zinaendelea ikiwemo kuboresha maeneo yanayotumika kwa ajili ya sherehe hizo kwa kuyajenga ili yawe ya kudumu.

# MAKATIBU WAKUU SJMT, SMZ WAJADILI MASUALA YA MUUNGANO




*Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) Balozi Dkt. Moses Kusiluka (kushoto) akiongoza kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023. Kulia ni Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said.*




*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Mary Maganga (kulia) akifuatilia kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Mary Maganga akisalimiana na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi, Bw. Xavier Daudi (kushoto) na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Kennedy Gastorn muda mfupi kabla ya kuanza kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023.*


# MAKATIBU WAKUU SJMT, SMZ WAJADILI MASUALA YA MUUNGANO



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akisalimiana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Bw. Ali Juma wakati wa kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam tarehe Septemba 22, 2023.*



*Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi (kulia) na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Dkt. Switbert Mkama wa pili kulia, wakifuatilia kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023.*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Bi. Mary Maganga (katikati) akiwa katika picha pamoja na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Dkt. Switbert Mkama (kushoto) na Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Bw. Abdallah Mitawi muda mfupi kabla ya kuanza kwa Kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023.*

# MAKATIBU WAKUU SJMT, SMZ WAJADILI MASUALA YA MUUNGANO



*Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) Balozi Dkt. Moses Kusiluka (wa pili kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) Mhandisi Zena Ahmed Said (wa pili kulia), Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga na Makatibu Wakuu kutoka SJMT na SMZ mara baada ya kumalizika kwa kikao cha kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023.*



*Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) Balozi Dkt. Moses Kusiluka (wa pili kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) Mhandisi Zena Ahmed Said (wa pili kulia), Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (kushoto), wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar mara baada ya kumalizika kwa kikao cha kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023.*

*Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Mitawi (katikati) akifurahia jambo na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba (kushoto) na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi, Bw. Xavier Daudi kabla ya kuanza kwa kikao cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023.*



# MAKATIBU WAKUU SJMT, SMZ WAJADILI MASUALA YA MUUNGANO



*Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wakifuatilia kikao cha cha Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujadili masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam Septemba 22, 2023.*



# Waziri Jafo ateta na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais (hawapo pichani) wakati akifungua kikao kazi kilichofanyika jijini Dodoma Agosti 3, 2023. Kulia ni aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Switbert Mkama.*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga akizungumza wakati wa kikao na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wakati wa kikao kazi kilichofanyika jijini Dodoma Agosti 3, 2023 kilichofunguliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo (kulia) na kushoto ni Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo amekutana na kuzungumza na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika kikao kazi kilichofanyika jijini Dodoma Agosti 3, 2023.

Akifungua kikao hicho, amesema kuwa ushirikiano baina ya viongozi na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais umechangia katika kudumisha Muungano na kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira.

Kutokana na hatua hiyo, Dkt. Jafo amewashukuru na kuwapongeza viongozi na watumishi kwa ujumla kusukuma mbele ajenda ya mazingira kupitia usimamizi wa kanuni na miongozi mbalimbali ya mazingira.

"Ndugu zangu watumishi nitoe pongezi za dhati kwenu kwani mmetumia vyema utaalamu wenu katika



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo (kushoto) akiagana Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga (wa tatu kushoto), aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Dkt. Switbert Mkama na Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Bw. Abdallah Hassan Mitawi na mara baada ya ufunguzi wa kikao kazi jijini Dodoma Agosti 3, 2023*



kusimamia vizuri hifadhi ya mazingira kupitia kampeni zetu mbalimbali za mazingira," amesisitiza.

Pia, Waziri Jafo amewahimzia wasimamizi wa miradi inayotekelezwa na Ofisi hiyo kuendelea kuisimamia vyema ili iendelee kueleta tija kwa wananchi katika maeneo yenye changamoto za mazingira.

Amewahimiza watumishi hao kuishi kwa kupendana na kutimiza wajibu wao kwa kufanya kazi kwa ufanisi na kwa kujituma ili kuacha alama nzuri.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga amewahimiza watumishi wa ofisi hiyo kuwa wabunifu ili kupata matokeo makubwa katika utekelezaji wa majukumu.

Pamoja na kuwapongeza watumishi hao, pia amewataka waendelee kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kwani kwa kufanya hivyo kutachangia katika kusukuma mbele maendeleo.

Pia, ametoa rai kwa watumishi kupitia ubunifu na taalama zao watumie fursa ya teknolojia inayopatikana ili kuboresha mazingra ya kazi na hivyo kufanya utendaji wa kazi kuwa wenye tija.

Aidha, Bi. Maganga amesema kuwa ana matarajio makubwa kutoka kwa watumishi hao kuona wanafanya kazi kwa bidii hatua itakayosaidia kuleta tija na matokeo mazuri.

# Kigahe aipa kongole Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuandaa kitabu cha Muungano

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe amepongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuandaa Kitabu cha Muungano ambacho kitasaidia kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kufahamu chimbuko, historia na mafanikio ya Muungano huo.

Mhe. Kigahe ametoa pongezi hizo Agosti 5, 2023 wakati alipotembelea Banda la Ofisi ya Makamu wa Rais iliyoshiriki katika maonesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.



*Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe akioneshwa kitabu cha Historia ya Muungano na Tanganyika na Zanzibar; Chimbuko, Misingi na Maendeleo na Afisa Maendeleo ya Jamii Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Zanipha Msangi alipotembelea Banda la Ofisi hiyo kwenye Maadhimisho ya Sikukuku ya Wakulima Duniani (Nanenane) katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 5, 2023. Katikati ni Bi. Habiba Mhina kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.*



*Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe akizungumza jambo na Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais alipotembelea Banda la Ofisi hiyo kwenye Maadhimisho ya Sikukuku ya Wakulima Duniani (Nanenane) katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 5, 2023.*

Mhe. Kigahe amesema Muungano ni tunu ya taifa ambao umeendelea kudumu kutokana na misingi ya imani, amani, umakini na usikivu wa Viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatua iliyowezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa baina ya wananchi wa pande zote mbili.

Aidha Naibu Waziri Kigahe ametoa wito kwa wananchi na viongozi kutimiza wajibu wa kuuenzi, kuudumisha, kuuimarisha na kuuendeleza Muungano kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo kwa kutoa elimu kwa vijana inayohusu historia, msingi na chimbuko la Muungano.

Kwa mujibu wa Mhe.Kigahe amesema Kitabu cha Muungano pindi kitakapoanza kufundishwa mashuleni kitakuwa nyenzo muhimu ya msingi wa maarifa na taarifa sahihi kwa wanafunzi kufahamu historia na mafanikio yaliyopatikana katika Muungano.

"Naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuandaa kitabu hiki ambacho kimekuja kwa wakati mwafaka kwani kitawezesha vijana wetu kuweza kujifunza na kuelewa kwa mapana historia ya Muungano wetu ambao umeleta mafanikio lukuki kwa wananchi wa pande zote mbili" amesema Mhe. Kigahe.

Kwa upande wake, Afisa Maendeleo ya Jamii Mkuu, Idara ya Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais Bi Zanifa Msangi alimshukuru Naibu Waziri Kihage kutembelea Banda la Ofisi hiyo kwani kupitia maonesho hayo elimu ya masuala ya Muungano na Mazingira imeendelea kutolewa kwa wananchi na wadau mbalimbali kwa ajili ya kukuza uelewa wa pamoja.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Kigahe amepongeza hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuhamasisha juhudi za utunzaji na uhifadhi wa mazingira kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191.

Ofisi ya Makamu wa Rais imeungana na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za umma na binafsi kushiriki Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya yakiongozwa na kauli mbiu isemayo ***"Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula"***




# Mitawi: Mradi wa SUSTAIN kuwa mwarobani wa upotevu wa misitu

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Bw. Abdallah Hassan Mitawi amesema kumekuwa na upotevu wa hekta 490 za misitu kila mwaka hivyo kusababisha hali ya jangwa, upungufu wa maji na chakula.

Amesema hayo Mei 23, 2023 jijini Mbeya wakati akizindua Mradi wa SUSTAIN Eco unaosimamiwa na Taasisi ya International Union for Conservation of Nature (IUCN) wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 4.5 sawa na shilingi bilioni 11.

Mradi huo utahusika na usimamizi shirikishi wa ikolojia katika masuala ya Serikali, biashara na jamii husika, ili kuleta uwiano katika vipaumbele na ukuaji endelevu.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Bw. Mitawi alisema Tanzania imekuwa ikiathiriwa na kutokuwepo kwa usawa wa bionuai na hivyo kusababisha kutokea kwa migogoro kati ya makundi mbalimbali hususan ya wakulima na wafugaji.

Hivyo, kutokana na hali hiyo amewataka wadau wengine kujihusisha na masuala ya mazingira akibainisha kuwa uhai wa binadamu na viumbe vingine vyote unategemea mazingira.

Ametoa shukrani kwa Serikali ya Sweden pamoja na Taadidi ya IUCN kwa kuonesha ushirikiano katika kuyajali mazingira jambo ambalo ni muhimu kwa ustawi wa nchi yetu.

Kwa upande wake Mkuu wa IUCN Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika Bw. Charles Oluchina ameishukuru Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuonesha ushirikiano mzuri katika usimamizi wa mazingira.

Pia, ameishukuru Serikali ya Sweden kwa kufadhili masuala ya mazingira na hasa Mradi wa SUSTAIN Eco akisema kuwa fedha hizo zitasaidia katika kubadilisha, kuhabarisha, kuimarisha matumizi ya rasilimali na kuzifanya ziwe endelevu.

"Usimamizi wa mazingira, bioanuai na mabadiliko ya tabianchi ni suala endelevu na kwa kuwa tarehe 22 mwezi Mei,2023 ilikuwa Siku ya Bionuai Duniani, hivyo uzinduzi wa mradi huu umefanyika kwa wakati muafaka," alisema Bw. Olunuchi.

Nae, Balozi wa Sweden nchini Tanzania Bi. Charlotte Ozaki Macias alisema kuwa mwaka 2023, Serikali ya Sweden inaadhimisha miaka 60 ya ushirikiano pamoja na Serikali ya Tanzania na kwamba 22/5/2023 ilikuwa siku ya maadhimisho ya bionuai bado kuna ongezeko la jangwa, upungufu wa maji, wanyama na viumbe vingine vinazidi kupungua.

Aliongeza kuwa ongezeko la watu duniani nalo, limechangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabianchi akisisitiza kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kuwe endelevu.

Mwakilishi wa Taasisi ya IUCN Tanzania ambaye pia Meneja wa Programu ya SUSTAIN ECo, Bw. Anthony Mhagama alieleza kuwa mradi huo ambao unasimamiwa na IUCN, utafanya kazi kwa kushirikiana na African Wildlife Foundation (AWF) pamoja na SNV katika katika maeneo matatu ambayo ni Kilombero, Katavi na Morogoro.

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS YATOA ELIMU KWA WANANCHI NANENANE MBEYA



*Mkurugenzi wa Idara ya Muungano Bi. Hanifa Selengu akitoa elimu ya kuhusu masuala ya Muungano kwa wananchi waliotembelea Banda la Ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya Agosti 6, 2023.*



*Afisa Mazingira Mwandamizi Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Martha Ngalowera ufafanuzi kwa wananchi waliotembelea Banda la Ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 4, 2023.*



*Afisa Mazingira Mwandamizi kutoka Idara ya Mazingira ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Lungo akitoa ufafanuzi kwa na wananchi Banda la Ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya Agosti 4, 2023.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Elisha Msengi akisaini kitabu cha wageni wakati alipofika katika Banda la Ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya Agosti 6, 2023.*

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS YATOA ELIMU KWA WANANCHI NANENANE MBEYA



*Afisa Maendeleo ya Jamii Mkuu kutoka Idara ya Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Zanipha Msangi akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari JM Kikwete iliyopo Tunduma Mkoani Mbeya wakati walipotembelea Banda la Ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 4, 2023.*

*Bi. Habiba Mhina kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari JM Kikwete iliyopo Tunduma Mkoani Mbeya wakati walipotembelea Banda la Ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 4, 2023.*





*Afisa Mazingira Mwandamizi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Evansia Shirima akitoa maelezo kuhusu elimu ya Muungano kwa kwa wanafunzi wa shule ya msingi Onical wakati walipotembelea Banda la Ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 6, 2023.*

*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Dynamic ya Jijini Mbeya wakiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais mara baada ya kutembelea Banda la Ofisi hiyo katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Duniani (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 4, 2023.*











**Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Ofisi ya Makamu wa Rais**
S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 266 235 2038 • Nukushi +266 235 0002
Barua pepe: km@vpo.go.tz • Tovuti: www.vpo.go.tz
Ofisi ya Makamu wa Rais blog.vpo.go.tz